# Nipashe

Alhamisi Septemba 10, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580334

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Mwalimu adaiwa kuuawa kwa risasi akiwa nyumbani kwake

UKURASA 5



ama

ALHAMISI SEPTEMBA 10, 2020

AFYA NA MAZINGIRA

Kijiji kinapojenga ofisi 'kali' kuliko DC, DED

'Majiko sanifu ya umeme ndiyo mwokozi pekee misitu'

UNICEF bega kwa bega upatikanaji, usambazaji chanjo ya COVID-19

AFYA

Na Sabato Kasika

NI BALAA SIGARA

•Inazichoma 30,000/- za mvutaji 'deile'

•Muhimbili yaitaja magonjwa ya moyo

Dk. Lutgardi Kagaruki, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF). PICHA: MTANDAO

UKURASA 11

# Lissu: CHADEMA imara kuliko 2015

**ASEMA** kampeni za kanda zimethibitisha, aweka wazi kumuunga mkono Maalim Seif Zanzibar... *Endelea uk. 2*



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad (kushoto), akirejesha fomu za kuomba uteuzi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, mjini Zanzibar jana. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ADC, Hamad Rashid Muhammed (kushoto), akirejesha fomu za kuomba uteuzi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, mjini Zanzibar jana.

## Magufuli aahidi mitaji kwa wachimbaji wadogo

UKURASA 3

## VIONGOZI CHADEMA MBARONI KWA MADAI MAUAJI

UKURASA 3

MICHEZO MO DEWJI: SIONDOKI SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu tathmini ya siku kumi za kampeni za chama hicho kikanda. Kulia ni msemaji wa chama hicho, Tumaini Makene. **PICHA: SALOME KITOMARI**

# Lissu: CHADEMA imara kuliko 2015

**Na Salome Kitomari**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema chama hicho kimezidi kuimarika kuliko mwaka 2015, licha ya misukosuko na dhoruba nyingi alizopitia kwa miaka mitano.

Akizungumza na wahariri na waandishi waandamizi wa vyombo vya habari jana jijini Dar es Salaam, alisema katika siku 10 kuzindua kampeni katika kanda 10 za chama hicho, wamebaini wananchi wana kiu ya maendeleo ndiyo maana wanakwenda kwenye mikutano hiyo kusikiliza sera zitakazowafikisha katika mabadiliko.

Alisema katika siku hizo, wameona idadi ya watu wanaowaunga mkono na kwamba imeonyesha chama hicho bado ni imara licha ya magumu mengi waliyopitia kwa miaka mitano.

"Watu anakuja kwa maelfu kwa sababu anataka kuja kutusikiliza, tathimini yetu inatwambia kuwa watu wanataka mabadiliko. Pamoja na kuenguliwa kihistoria kwa wagombea wetu, waliobaki wa ubunge na udiwani wana nafasi kubwa sana za kushinda. Hadi jana wagombea ubunge 55 na 1,025 wa udiwani walioenguliwa wamekata rufani wanasubiri," alisema.

"Baada ya vita ya miaka mitano dhidi ya CHADEMA ya watu kuzuiwa kufanya siasa, ilitazamiwa tuwe tumeshakufa na kuna baadhi walikuwa wanasema CHADEMA kwisha. Enguaengua hii inathibitisha CHADEMA ina nguvu zaidi leo kuliko ilivyokuwa maka 2015," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, mwaka huu waliweka wagombea ubunge 244 kati ya majimbo 264 ya Bara na majimbo 30 ya Zanzibar na kati ya kata 3,955 waliweka wagombea 3,754 na kwamba hawakuweka kwenye kata 201 pekee.

"Haijawahi kutokea katika historia yetu yote kuwa na nguvu kubwa namna hii kwenye uchaguzi kama tuliyo nayo mwaka huu ambayo inaonyesha tuna nguvu kuliko ilivyokuwa miaka mitano iliyopita. Tunaungwa mkono na watu wengi kuliko miaka ya nyuma," alisema.

"Hii ndiyo maana nasema kuna uwezekano mkubwa mwaka huu tukaishinda CCM pamoja na kila ugumu ambao tumewekewa. Wagombea wetu kila mahali wamejiandaa vizuri sana. Tuko vizuri sana pamoja na matatizo yetu yote ya kifedha na kuenguliwa kwa wagombea wetu tuko vizuri sana," aliongeza.

Pia alisema uchaguzi wa mwaka huu si rahisi na kwamba alishiriki uchaguzi wa mwaka 2015 na kwamba anafahamu jinsi uchaguzi ulivyo amgumu kwa chama cha upinzani kutokana na mifumo ambayo wateule wa Rais ndio viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kwa mujibu wa Lissu, Makamishna na watendaji wa NEC ni wataule wa Rais, watumishi wa umma ambao wanaweza kufukuzwa kazi wakati wowote na kwamba mfumo mzima wa uchaguzi hauko huru na haujawahi kuwa huru, pamoja na vyombo vya dola na kwamba wanategemea uamuzi wa wananchi katika sanduku la kura.

**UKATA**

Lissu alisema chama hicho kinaomba michango kwa sababu hali ya uchumi ni mbaya, na kuwaomba Watanzania kuachangia Sh. 100 kila mmoja ambayo itawawezesha kufanya kampeni.

"Uchumi ukiwa mbaya ishara utaiona kwenye kampeni, huoni mabango kwasababu hakuna fedha. Tunachangisha kwa sababu tunataka watu watusaidie, nimefukuzwa kazi (Ubunge) sijalipwa kiinua mgongo changu, lazima niombe mchango nifanye kampeni,"alisema.

"Hali ya kampeni kifedha siyo nzuri na tunataka wananchi waelewe na watuchangie, namna ya kufikisha kampeni salama tutahitaji kila mmoja ajiongeze atuchangie Sh. 100,"alisema.

**WAMWANGUKIA MEMBE**

Aidha, alisema chama hicho kitamuunga mkono mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharf Hamad, kwa kuwa ndiye anayekubalika na anaweza kumshinda mgombea wa CCM.

Pia, kimekiomba ACT Wazalendo kukiunga mkono Chama hicho kwa upande wa Tanzania bara kwa kuwa ndiyo chama chenye nguvu.

"Mazungumzo na ACT-Wazalendo hayajafa ila tumesema Maalim Seif ndiye anaweza kuishinda CCM na ndiyo tutawaunga mkono asilimia 100, sisi tunaweza kuokoteza kura lakini hatutaweza kuishinda CCM Zanzibar, wagombea wetu tumewataka wamuunge mkono, si msimamo wa Lissu bali wa CHADEMA,"alisema.

"Ukiangalia Bara kwa macho angavu anayeweza kuishinda CCM ni CHADEMA, Tumependeza kwa wenzetu atuachie upande wa bara, hatusemi waachie kila kitu bali yale maeneo ambayo atashinda waendelee, tusigombee kiti kama abiria wa Titaniki, kikubwa tushinde uchaguzi Bara na Zanzibar alafu tutakaa tuzungumze,"alifafanua.

**BARAZA LA MAWAZIRI**

Alisema CHADEMA inataka kubadili mfumo wa utawala na watafuata mfumo uliopo kwenye rasimu ya katiba ya Jaji Joseph Warioba, ili kuepukana na serikali ya gharama ambayo inawagharimu walipa kodi, na atakuwa na mawaziri 14.

**KUTUMIWA NA MABEBERU**

Alisema kumekuwa na maneno kuwa anatumia na mabeberu na kutaka kutajiwa ni kina nani hao, na kama ni mataifa yaliyoendelea kama Marekani, ndiyo anatoa misaada ya maendeleo kwenye afya na kufundisha vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi. "Hizi ni nchi rafiki wa Tanzania tangu enzi za Mwalimu (Julius) Nyerere. Nikiingia madarakani tutawarudia marafiki zetu wote na kurejesha uhusiano ambao kwa sasa umetetereka. Tunawaita mabeberu huku tunawaomba misaada ya elimu, afya na wanamiliki migodi mikubwa nchini," alisema.

# ACT yaitaka NEC iweke wazi majina ya walioshinda rufani

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuweka hadharani majina ya wagombea wote wa ubunge na udiwani walioshinda rufani zao baada ya kuenguliwa na wasimamizi wa uchaguzi.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana,kuhusu taarifa iliyotolewa na NEC kwa umma ya kuwarejesha baadhi ya wagombea walioenguliwa, ilieleza kuwa haijitoshelezi kwa kuwa haikuweka bayana majina au majimbo ambayo tayari rufani zake zimefanyiwa kazi.

Chama hicho kilidai kuwa jambo hilo linasababisha wagombea husika kushindwa kuendelea na kampeni kutokana na kukosa uhakika wa ama kurejeshwa au kutorejeshwa.

Juzi, NEC bila kutaja majina yao, vyama vyao na majimbo wanakotoka, ilitangaza kwa kati ya rufani 55 zilizopitiwa hadi kufikia juzi, 15 zilikubaliwa na wagombea kurejeshwa katika orodha.

Jana, NEC ilitangaza kuwarejesha wagombea ubunge wengine 13 walioenguliwa na wasimamizi wa uchaguzi na 14 waliowekewa mapingamizi baada ya kuteuliwa.

Katika taarifa yake ya jana, tume hiyo ilisema wagombea waliorejeshwa ni wa majimbo ya Singida Magharibu, Madaba, Ilemela, Namtumbo, Bagamoyo, Liwale, Tunduma, Bukene na Kigamboni.

Kurejeshwa kwa wagombea hao 13 kunafanya idadi ya waliorejeshwa kuwa 28 tangu kuanza kutolewa uamuzi wa rufani zao juzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi rufani 34. Kati yake, 13 zimekubaliwa na kurejesha wagombea hao.

Hata hivyo, alisema tume hiyo imekataa rufani saba za wagombea ambao hawakuteuliwa kwenye majimbo ya Singida Magharibi, Bahi, Handeni Vijijini, Madaba, Singida Mashariki, Ileje, Meatu na Bukene.

Dk. Charles alisema NEC pia imekataa rufani 14 za kupinga kuteuliwa ambazo zinatoka kwenye majimbo ya Mwanga, Mafinga, Ilala, Manonga, Igunga na Kisesa.

"Idadi hii inafanya jumla ya rufani za wagombea ubunge zilizofanyiwa uamuzi na tume kufikia 89. Hii inafuatia taarifa iliyotolewa jana (juzi) ambapo tume ilitangaza uamuzi wa rufani 55,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema tume hiyo inaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufani hizo kila siku na wahusika watajulishwa kwa barua juu ya uamuzi huo.

Septemba 8, mwaka huu, NEC ilianza kazi ya kuchambua na kuzifanyia kazi rufani 557 za wagombea hao, ikiwarejesha wagombea 15 kati ya 55 na kukataa rufani 40 kwa sababu mbalimbali.

# Viongozi CHADEMA mbaroni tuhuma za mauaji kada wa CCM

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

WATU wanne akiwamo Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Songwe, Isakwisa Lupembe, na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Ally Mwafongo, wamekamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za mauaji ya kada wa CCM, Brighton Mollel.

Watuhumiwa wengine waliokamatwa wakituhumiwa kuhusika na mauaji hayo yaliyotokea Agosti 25, mwaka huu, mjini Tunduma Flowin Mwalongo na Moses Mshani.

Mollel aliuawa baada ya kuzuka vurugu kati ya watu wanaodaiwa kuwa wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CHADEMA katika ofisi za kata ya Mwaka mjini Tunduma.

Vurugu hizo zilitokea wakati maofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakibandika majina ya wagombea udiwani wa kata hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, akizungumza na gazeti hili jana, alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kuungana na wenzao 16 ambao tayari wamefikishwa katika chombo hicho cha sheria na kusomewa shtaka la mauaji.

Kamanda Kyando alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa mafichoni wilayani Kyela, mkoani Mbeya ambako inadaiwa walikimbilia huko baada ya tukio hilo la mauaji kutokea.

"Mimi sipendi kutaja wadhifa wa mtu maana uhalifu hauna uhusiano na wadhifa wa mtu. Lakini yeyote aliyefanya kitendo kile bila kujali wadhifa wake kwenye chama chochote sisi kwetu ni mhalifu kama mhalifu yeyote na tunaendelea kuwatafuta wote waliohusika," alisema Kyando.

Alisema mbali na watu hao kukamatwa, bado jeshi hilo linaendelea kuwasaka watu wengine wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji hayo ambao wanadaiwa kukimbilia nchi jirani.

Baada ya mauaji hayo kutokea, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas, alifika mkoani Songwe na kuagiza watu wote waliodaiwa kuhusika katika mauaji hayo wasakwe popote pale walipo na kukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.



Mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa Kahangalala, mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

# JPM aahidi mitaji wachimba madini

**Na Gwamaka Alipipi,** GEITA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaahidi neema tano wachimbaji wadogo wa madini endapo atachaguliwa tena kuongoza nchi.

Amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, wachimbaji wa madini watatengewa maeneo maalumu ya uchimbaji, kuwapatia leseni, mafunzo, mitaji na teknolojia.

Dk. Magufuli alitoa ahadi hiyo jana wakati akihutubia wananchi waliojitokeza kumsikiliza kwenye Uwanja wa Kalangalala mkoani Geita.

Alisema kuwa lengo kuu ni kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kufanya shughuli zao kwa tija na urahisi.

"Wachimbaji wadogo walikuwa wanafukuzwa pindi wakigundua eneo la madini, lakini leo wakigundua wanapewa leseni, wanaendelea na uchimbaji. Sasa tumewaandalia mazuri zaidi na hayo yote yasipotee ndugu zangu ninaomba mnichagure tena," alisema.

Kuhusu mafanikio katika sekta ya madini, Dk. Magufuli alisema mwaka 2016 wachimbaji wadogo walizalisha kilo 337.482 za dhahabu yenye thamani ya Sh. bilioni 22.5 na serikali kupata mrabaha wa Sh. bilioni 1.2.

Alisema baada ya serikali kuweka udhibiti katika sekta hiyo, mwaka jana yalipatikana madini kilo 4,656.29 yenye thamani ya Sh. bilioni 375.5 yaliyoiwezesha serikali kupata mrabaha wa Sh. bilioni 22.5.

Mwaka 2016, alisema yalipatikana madini kilo 17,587 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 607.3 (Sh. trilioni 1.4), hivyo serikali kupata mrabaha Dola za Marekani milioni 23.4 (Sh. bilioni 53.81).

Aliongeza kuwa mwaka 2020, yalipatikana madini kilo 21,652.77 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 949.8 (Sh. trilioni 2.2), serikali kupata mrabaha Dola za Marekani milioni 56.8 (Sh. bilioni 130.64).

"Haya mambo ndiyo najivunia kuwa Tanzania ni tajiri, tusingebana tusingeyapata haya yote. Tangu tutawaliwe tumepoteza kiasi gani? Haya ndiyo mambo ya msingi tumapaswa kujiuliza. Hata wagombea wenzangu wanapaswa kujiuliza," alisema.

**KUPANUA UTALII**

Aidha, Rais Magufuli alisema mipango ya serikali ni kuhakikisha kila ukanda wa Tanzania unakuwa na vivutio vya utalii, lengo likiwa ni kupata fedha nyingi za kigeni.

"Tunataka kila zone (kanda) ya nchi iwe na utalii. Tunataka Kanda ya Ziwa iwe na utalii na ndiyo maana tumeanzisha hifadhi ya Burigi-Chato, tunataka Mbeya, Iringa kote nchini kuwe na utalii siyo ukanda wa kaskazini peke yake," alisema Magufuli.

**KILIMO, UVUVI, UFUGAJI**

Dk. Magufuli alisema miaka mitano ijayo, serikali imeweka mkakati wa kuwanufaisha wakulima, wavuvi na wafugaji.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano serikali imefuta tozo 114 kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji. Alisema ujenzi wa mchinjio ya kisasa ni moja ya kipaumbele kwa miaka ijayo.

**MAKUSANYO KUPAA**

Aidha, Dk. Magufuli alisema matarajio ya serikali ni kuongeza makusanyo ya kodi ili kuwezesha ujenzi wa miradi ya maendeleo na ulipaji wa mishahara. Alisema: "Kwa kipindi cha miaka mitano, makusanyo ya kodi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 800 hadi Sh. trilioni 1.5 kwa mwezi. Gawio limeongezeka kutoka Sh. bilioni 161 hadi Sh. trilioni 1.528. Madini makusanyo kutoka Sh. bilioni 160 hadi Sh. bilioni 528, Halmashauri makusanyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 379 hadi Sh. bilioni 713."

# ...Ataka mataifa kujifunza kwa Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi,** GEITA

RAIS John Magufuli, ameyashauri mataifa ya kigeni kuja nchini kujifunza Mungu alivyofanya maajabu ya kuutokomeza ugonjwa wa virusi vya corona.

Amesema wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo, nchi mbalimbali duniani zilimsahau Mungu, lakini Tanzania ilimwomba na kufanikiwa kuutokomeza.

Rais Magufuli alitoa ushauri huo jana mkoani hapa wakati akihutubia wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza katika Uwanja wa Kalangalala.

"Tanzania tuna uhuru, makanisa ruksa, misikiti ruksa, nchi zingine hata uhuru wa kuabudu haupo. Mnakumbuka hata wakati wa ugonjwa wa corona mataifa mengine yalifunga misikiti na makanisa, sisi tukasema hapana, tukasema tumwombe Mungu na kwenye matatizo Mungu hashindwi," alisema na kuongeza:

"Baada ya maombi ugonjwa wa corona ukaenda kwa wengine huko, tumshangilie Mungu kwa kupiga miluzi. Mungu hoyee. Hayo ndiyo maajabu ya Mungu katika nchi yetu. Ndiyo faida ya kumtanguliza Mungu, watu wengine waje wajifunze Tanzania namna ambavyo tumefanikiwa."

Aidha, Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali imetumia Sh. trilioni 37.8 katika kutekeleza miradi ya maendeleo nchini.

Alisema katika kiasi hicho, miradi mikubwa kama vile bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere na reli ya kisasa imejengwa.

Katika kipindi cha miaka mitano, alisema serikali imedhibiti utoroshaji wa madini, ujenzi wa masoko ya madini na rasilimali kuwanufaisha Watanzania,

Kuhusu mafanikio mkoani Geita, alisema serikali imejenga hospitali za wilaya nne na watumishi wa afya 192 wameajiriwa.

"Kwenye elimu tumefanikiwa kujenga madarasa 1539, nyumba za walimu 162 pamoja na kutoa Sh. bilioni 35.3 kwa ajili ya elimu bure, vijiji 282 vimefikiwa na umeme, pamoja na Sh. bilioni 36.5 kutumika kuleta huduma ya maji," alisema Rais Magufuli.

Alisema katika mkoa wa Geita kuna viwanda 926, vikubwa ni viwili, vya kati ni vinne na vidogo ni 920.

Rais Magufuli alisema zaidi ya Sh. bilioni 130 zimetengwa kwa ajili ya kuleta huduma ya maji mkoani Geita, Sh.bilioni 73.2 kwa ajili ya kuzipatia kaya maskini.

Aidha, alisema miaka mitano ijayo serikali itajenga barabara kutoka Geita hadi Kahama kwa kiwango cha lami.

"Baadhi ya mafanikio ambayo yamepatikana mkoa wa Geita, ili mjue mlikotoka, mlipo na mnakokwenda. Geita ni mkoa ambao umebarikiwa kwa kuwa rasilimali nyingi, katika madini kumekuwapo na jitihada za kusimamia rasilimali ya madini, hivyo kwa Geita limeanzishwa soko kubwa la madini, imetungwa sheria ya madini, na kuanzisha masoko," alisema Dk. Magufuli.

Naye Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Geita, Alhaji Said Kalidushi, alisema kwa miaka mitano mkoa wa Geita umekuwa kinara wa kutengeneza fursa za kimaendeleo.

Alisema kwenye idara ya afya, tangu mwaka 2015 zimejengwa hospitali nne ikiwamo hospitali ya wilaya ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilika.

Kalidushi alisema: "Nakuahidi Geita hatutakuangusha, dunia inashuhudia maendeleo makubwa yanayofanyika nchini na Geita ikiwamo."

# CHAUMMA kuruhusu wagombea huru

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

CHAMA cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), katika ilani yake kimebainisha kuwa ikiwa wananchi watakipa ridhaa ya kuongoza, miongoni mwa mambo ambayo kitayafanya ni kuruhusu wagombea huru wa urais, ubunge na madiwani.

Mgombea urais kupitia chama hicho, Hashim Rungwe, tayari amezindua kampeni zake Septemba 5, mwaka huu, eneo la Manzese Bahkresa jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ilani ya chama hicho, serikali ya CHAUMMA itahakikisha rasimu ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania iliyojadiliwa katika bunge maalumu la katiba la mwaka 2014 inarejeshwa kwa utekelezaji kama ilivyopendekezwa na wananchi.

Katika agenda hiyo, CHAUMMA imesema itaweka sheria mpya za uchaguzi zitakazowawezesha wananchi kupata haki kwa kuanzisha mahakama ya kudumu ya katiba itakayopokea na kusikiliza masharti ya kikatiba, raia binafsi au taasisi.

Ilani hiyo pia imeeleza kuwa itatenganisha madaraka ya Rais wa Muungano, Rais wa Tanzania Bara na Rais wa Zanzibar na itaruhusu wagombea huru wa nafasi ya udiwani, ubunge na urais.

Katika kipengele cha kutokomeza ufisadi na rushwa, CHAUMMA imeeleza kuwa itatengeneza vyombo vyenye nguvu kubwa na mtandao ulioenea nchi nzima, chombo chenye meno makali ya kutokomeza ulaji rushwa kiutendaji, kuandaa muswada wa sheria itakayotoa adhabu kali zaidi kwa walaji na watoa rushwa na kufuta mara moja mikataba yote iliyosainiwa katika mzingira ya kifisadi.

Kuhusu sekta za kiuchumi, chama hicho kimedai kuwa kitakuwa na mkakati wa makusudi wa kimarisha uchumi kwa kuhakikisha mauzo ya bidhaa nchi za nje yanaongezeka kwa asilimia kubwa na kupunguza bidhaa kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani.

Aidha, imesema serikali ya CHAUMMA itaandaa mikopo ya fedha kwa wahitimu kutoka vyuoni na shuleni na kuanzisha miradi mbalimbali ya uchumi ndani na nje ya nchi na itaongeza pensheni za wastaafu ili wastaafu wapate kiwango cha asilimia 80 ya mishahara yao.

Ilani hiyo imeeleza kuwa katika kuboresha uchumi wa nchi, kitajenga viwanda vya zana za kisasa za kilimo na mifugo, kutoa ruzuku kwa wafugaji na wakulima na fidia au upendeleo katika kodi kwa ajili ya kuendeleza kilimo na mifugo, kujenga viwanda vya kusindika bidhaa za kilimo na mifugo na kufufua huduma za ughani katika kilimo na mifugo.

Kuhusu mawasiliano na uchukuzi, kimesema kitajenga barabara kwa kiwango cha lami, ili kuhakikisha kuwa kila makao ya halmashauri yanafikika kwa barabara ya lami na kujenga mfumo mpya wa usafiri wa barabara na reli katika miji mikubwa ikianzia Dar es Salaam ili kuondoa kero ya msongomano wa magari uhaba wa usafiri na kuondoa ajali zinazosababiswa na barabara mbovu na nyembamba.

Katika uwekezaji, CHAUMMA imesema itaweka msharti ya uwekezaji yanayohakikisha kuwa wawekezaji wageni wanakuza ajira, uzoefu na teknolojia kwa wananchi na pia wanabakiza kiasi cha kuridhisha cha mapato nchini kwa kuwekeza upya faida yao katika miradi mengine mipya.

Kwa upande wa elimu, serikali ya CHAUMMA itabadili mitaala ya elimu kwa kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu, ili kuipa ubora wa hali ya juu na maudhui na vionjo vya kitanzania na kimataifa.



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# JK akoleza moto kampeni za CCM

**Na Said Hamdani, LINDI**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, amekoleza moto kampeni za Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku akisema Watanzania wanapaswa kuendelea kukiamini chama hicho ili kushika dola.

Amesema CCM inastahili kupewa tena nafasi ya kuongoza ili kuwatumikia wananchi na kudumisha amani, upendo na kuwaletea maendeleo wanayoyahitaji.

Sambamba na hayo, Kikwete aliwaomba wananchi kutokubali kuyumbishwa na maneno ya wapinzani kwa kile alichodai wameishiwa hoja kwa kuwa yote wanayosema ni yale yaliyopita, ambayo CCM imeshayafanya muda mrefu.

Kikwete alitoa ahadi hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni kwa nafasi za ubunge na udiwani mkoa wa Lindi, zilizofanyika katika uwanja wa Ilulu mjini hapa.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano, mgombea urais wa CCM, Rais John Magufuli amefanya mambo mengi mazuri ya kimaendeleo, ikiwamo uboreshaji huduma za afya, elimu, nishati na utoaji mikopo kwa vijana na kinamama.

Katika kipindi hicho, alisema kwa mkoa wa Lindi pekee zimejengwa hospitali mbili za wilaya, vituo vya afya 16 na zahanati 70 zimeboreshwa katika halmashauri zote sita.

Licha ya uboreshaji wa huduma hizo, pia alisema mikopo 4,693 yenye thamani ya Sh. 2,313,534,500 imetolewa kwa vijana, kinamama, na watu wenye uhitaji maalum kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na halmashauri za wilaya na manispaa.

"Kipindi cha miaka mitano tu CCM imeyafanya yote hayo. Naomba mtupe tena miaka mitano mingine tukamilishe mambo na miradi iliyobaki," alisisitiza Kikwete.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa kinu cha kuchakata gesi asilia, aliwaomba wananchi kuendelea kufanya subira kwa kuwa serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni za Equinol na State Oil na yatakapokamilika kazi ya ujenzi itaanza mara moja. Alisema mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 30, umepangiwa kujengwa eneo la Likong'o, Manispaa ya Lindi tayari serikali imeshalipa fidia kwa wakazi ambao mradi huo utapita. "Hivi kama uwekezaji haupo kulikuwa na maana gani kulipa wananchi fidia?" Alihoji Kikwete.

## Mgombea ajinadi kurejesha shuleni watoto waliopata ujauzito

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salome Makamba, amezindua kampeni za kuwania nafasi hiyo, huku akiahidi kupigania waliopewa ujauzito kurejeshwa shuleni iwapo atashinda.

Makamba alibainisha hayo juzi kwenye viwanja vya Ngokolo mjini hapa katika mkutano uliojumuisha wagombea udiwani kutoka kata 17, wapenzi, wanachama na viongozi wa chama.

Mkoa wa Shinyanga, alisema unaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kitaifa kwa asilimia 59, hali ambayo imesababisha wanafunzi wa kike kuzima ndoto zao kwa sababu ya kuozeshwa na wengine kupewa ujauzito na kuacha masomo.

Alisema moja ya sera kwenye kampeni zake ni kupambana kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, tatizo alilosema limekuwa likizima ndoto za wanafunzi wa kike.

Makamba aliwaomba wananchi wamchague ili aka-ongeze nguvu ya mapambano akiwa bungeni pamoja na kupeleka hoja binafsi ya kutetea wanafunzi waliopewa ujauzito kurudi shuleni.

"Mimi kama mgombea ubunge mwanamke nina uchungu sana na wanafunzi ambao wamekuwa wakipewa ujauzito na kuzima ndoto zao kwa kuacha masomo, hivyo mkinichangua kuwa mbunge wenu nitakwenda bungeni kupigania wanafunzi hawa wawe wanarudi shuleni kuendelea na masomo," alisema Makamba.

"Nazungumza hivi kwa sababu gani kuna wanafunzi wengine walipewa ujauzito kwa kubakwa na haikuwa dhamira yao kuzima ndoto zao," aliongoza.

Makamba pia alisema akiwa mbunge atahakikisha mkoa wa Shinyanga unakua kimaendeleo kwa kuendana na utajiri ulio nao wa madini ya dhahabu na almasi, tofauti na ulivyo hivi sasa hauna hadhi kabisa na ni mkoa wa tano kitaifa unaochangia pato la taifa.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (BAVICHA) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Samson Ng'wagi, akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni, aliwataka wanawake wasimwangushe Makamba bali wakampigie kura za ushindi siku ya uchaguzi ili awe mbunge wao na kutetea maslahi yao ikiwamo kuboresha huduma za afya.

# Mwalimu auawa nyumbani kwake

**Na Pendo Thomas,**
KIGOMA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Kihenya, wilayani Kasulu mkoani Kigoma, ameuawa kwa kupigwa risasi na watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi akiwa nyumbani kwake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema tukio hilo limetokea Septemba 6, majira ya saa tatu usiku, baada ya watu hao kuvamia nyumba ya mwalimu Fredrick Richard (30), aliyekuwa akiishi na mke na watoto wawili.

Alisema watu hao hawakuongea neno lolote baada ya kuingia ndani, walimpiga risasi mwalimu huyo na kuondoka bila kuchukua kitu chochote.

Jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja akihusishwa na mauaji hayo baada ya polisi kuokota kofia katika eneo la tukio iliyosaidia kumpata mtuhumiwa huyo huku watuhumiwa wengine wakiendelea kutafutwa ili waunganishwe na mwenzao.

Kamanda alisema huenda tukio hilo ni la kulipa kisasi kwa kuwa wahalifu baada ya kutekeleza mauaji hawakuiba, hivyo kuwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi.

"Nitoe wito kwa wananchi wa Kigoma waache kuchukua sheria mkononi kwa kuwa kitendo hicho cha mauaji ya mwalimu kinadumaza jitihada za kuinua kiwango cha elimu," alisema.

Pia alisema kufuatia msako walioundesha wamefanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu 21 na kuwakabidhi kwa Uhamiaji ili taratibu zingine ziendelee.

Kamanda Manyama alisema hali ya ulinzi na usalama kwa Mkoa wa Kigoma kwa sasa ni shwari hivyo wananchi waishi kwa amani na wawe mstari wa mbele kusaidiana na jeshi hilo kutoa taarifa vinapotokea viashiria vya uhalifu.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kujenga kivuko kwa ajili ya waenda kwa miguu katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mgombea ubunge aibuka hoja ujenzi chuo ufundi

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MGOMBEA ubunge Jimbo la Bagamoyo kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Muharami Mkenge, amewaomba wananchi kumpa kura nyingi, ili asimamie ujenzi wa chuo cha ufundi kujengwa wilayani hapo.

Muharami amesema, tayari ombi hilo amemweleza mgombea mwenza wa urais wa CCM, Samia Suluhu Hassan, alipofanya mkutano wa kampeni hivi karibuni jimboni Bagamoyo.

Mkenge aliyasema hayo jana katika mkutano wake wa kampeni, kwenye uwanja wa Mgonela Kata ya Dunda. Alisema chuo cha ufundi kitakuwa suluhisho kwa vijana kupata ajira kwenye viwanda vinavyojengwa.

Alisema mbali na ombi la ujenzi wa chuo, pia alimkabidhi Samia ombi la ujenzi wa barabara ya Makofia mpaka Sunguvuni, ili kuyawezesha magari yanayopeleka dawa kwenye chanzo cha maji cha Ruvu Chini yaende wakati wote.

"Nawaomba wana Bagamoyo wenzangu mnipe ridhaa ya kuwa mbunge wenu. Nitafuatilia ujenzi wa chuo cha ufundi, na ujenzi wa barabara, kila eneo ili lifikike kwa urahisi bila kujali wakati wa masika au kiangazi," alisema.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Shukuru Kawambwa, aliwaomba wananchi kumchagua Mkenge, ili aendeleze yale yaliyoanzishwa na kwamba ana imani na mgombea urais wa CCM, Rais John Magufuli, endapo atachaguliwa atasimamia mambo ya mgombea huyo.

Awali, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abdul Sharifu, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kumchagua kwa kura nyingi Rais Magufuli, Mkenge na wagombea udiwani wa chama hicho, ili walete maendeleo na kuendeleza miradi ya kimkakati iliyoanzishwa.

# Lipumba ajinadi na mapinduzi ya kilimo

**Na Boniface Gideon,** KIBAHA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, ameahidi kuendeleza sekta ya kilimo na kurahisisha biashara ya mazao ya kilimo.

Prof. Lipumba alitoa ahadi hiyo jana wakati wa mikutano yake ya kampeni katika wilaya za Kibaha na Bagamoyo mkoani Pwani.

Alisema atatekeleza ahadi yake hiyo kwa kurekebisha mfumo wa kodi na ushuru wa mazao ya kilimo ikiwamo kufuta ushuru na ada zote za mazao kwa mkulima endapo atapata ridhaa ya Watanzania ya kuwa rais.

Prof Lipumba alisema kuwa kutokana na sera yake ya haki sawa na furaha kwa wote, chama hicho kina lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuutokomeza umaskini na kuchochea maendeleo ya viwanda kupitia sekta ya kilimo.

Prof. Lipumba alisema ikiwa atachaguliwa ataunda serikali ya umoja wa kitaifa ambayo itakuwa chini ya CUF, na kwamba itahakikisha taaluma ya ubwana/ubibi shamba inarejeshwa hadhi yake ikiwamo kuwawezesha maofisa ugani ili wafanye kazi zao katika viwango vinavyotakiwa na vyenye tija kwa wakulima nchini.

Aliongeza kuwa zaidi ya robo tatu ya Watanzania wanategemea sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, lakini kumekosekana sera sahihi ya kukuza kilimo na kuinua hali za maisha ya wakulima kwa kuwa zana za kilimo na pembejeo hazifikii, na hata zinapowafikia zinakuwa zimechelewa.

"Wakulima wa mikoa ya pwani wameachwa solemba bila msaada wowote, tunahitaji kuibadilisha hali hii.... ardhi ya pwani ni moja kati ya ardhi zinazokubali kilimo chochote pamoja na zao la korosho, lakini matokeo yake mmeachwa solemba," alibainisha.

Alisema utafiti katika nchi nyingi zilizoendelea unaonyesha kuwa kasi ya kukua kwa uchumi na uzalishaji katika sekta ya kilimo kunapunguza umaskini kwa kasi kubwa kuliko ukuaji wa sekta nyingine yoyote katika mataifa hayo.

Aidha, alisisitiza kuwa serikali yake ya umoja wa kitaifa itahakikisha kila halmashauri inajenga mazingira ya kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kusindika na kuyaongezea thamani mazao yanayozalishwa na wananchi katika halmashauri husika.

"Utaratibu huu siyo kwamba utawasaidia wazalishaji wa vijijini kuwa na soko ambalo liko tayari bali pia utasaidia sana katika suala zima la kuongeza ajira nchini kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya FAO, benki ya dunia na taasisi za utafiti wa kilimo," alieleza na kuongeza:

"Pia serikali ya kitaifa chini ya CUF itafanya utafiti wa kina juu ya mazao mengine ya biashara yanayoweza kustawishwa maeneo mbalimbali nchini."

Alisema baada ya utafiti huo kuyajua maeneo ya kustawisha pamoja na mazao husika, itarahisisha kutambua maeneo ya nchi yanakoweza kukuzwa na kwamba Serikali yake itatoa msaada kwa wakulima wa maeneo husika ili waweze kuyakuza pamoja na kuwatafutia wabia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sote tukumbuke kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi

**MAANDALIZI** ya Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu yako katika hatua muhimu ya kampeni; kwa maana fursa kwa vyama vya siasa na wagombea kuwaendea wananchi kwa lengo la kuwaomba kura.

Wagombea na vyama vyao wanatumia njia mbalimbali za kuwafikia wananchi (wapigakura), zikiwamo kampeni kwenye majukwaa, kwenye maeneo ya mikusanyiko, vikao vya ndani na hata makongamano pamoja na midahalo, ingawa kwa mwaka huu hatujashuhudia utaratibu wa midahalo.

Ikumbukwe kuwa kampeni ni mchakato muhimu pengine kuliko mingine ya uchaguzi kwa sababu ndipo wananchi wanapochukua uamuzi wa ni nani wamchague siku ya uchaguzi.

Uamuzi huo unafikiwa baada ya wapigakura kusikiliza na kuridhishwa na ilani, sera, mikakati na mipango ya vyama vya siasa na wagombea wake katika kuwaletea maendeleo.

Wakati huu ambao kampeni zimeshika kasi kwa baadhi ya vyama, pia vyama hivyo vinatumia kila njia kuhakikisha vinakubalika kwa wapigakura ili viaminiwe, hivyo kupata ridhaa Oktoba 28.

Tunaendelea kuhimiza na kuvisisitiza vyama, wagombea, wanachama na wafuasi kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na maelekezo kutoka katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), tukiamini kuwa kwa kufanya hivyo, uchaguzi huo utafanyika katika mazingira ya utulivu. Aidha, tunavikumbusha vyombo vya ulinzi na usalama hususan Jeshi la Polisi kuhakikisha linazingatia hayo kwa kuwa ndicho chombo chenye dhamana ya kusimamia usalama.

Ikumbukwe kuwa Jeshi la Polisi linawajibika kutoa ulinzi katika mikutano ya kampeni, kuwalinda wagombea pamoja na kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanakuwa na usalama uhakika kipindi chote cha uchaguzi.

Kutokana majukumu hayo mazito, tunalishauri jeshi hilo kuhakikisha linatekeleza majukumu yake kwa usawa bila kupendelea au kuegemea chama kimoja. Kwa upande wa NEC, tunaamini kuwa itaendelea kutimiza majukumu yake ya msingi ya kusimamia na kuratibu mchakato mzima wa uchaguzi kwa kuhakikisha kuwa inatoa haki kwa vyama vyote. Tume imepewa mamlaka ya kisheria kutekeleza majukumu yake kuanzia mchakato wa uandikishaji wapigakura, utoaji wa fomu kwa wagombea, uteuzi, kuratibu kampeni, kusimamia upigaji kura na kutangaza matokeo.

NEC imeshatekeleza jukumu la uandikishaji wa wapigakura kupitia uhakiki wa daftari la wapigakura, kutoa fomu kwa wagombea huku ikiendelea kuteua wagombea, wakati huo ikiendelea kushughulikia mapingamizi.

Ni matarajio yetu kwamba NEC inashughulikia mapingamizi yote yaliyowasilishwa kwake kwa wakati mwafaka, ili walioweka na kuwekewa mapingamizi wanapewa haki yao inavyostahili kisha walioshinda waanze kampeni.

Licha ya suala zima la uteuzi wa wagombea kuibua mjadala na malalamiko katika maeneo mengi hususan kutoka vyama vya upinzani, lakini bado tunaendelea kuamini kuwa NEC itatekeleza wajibu wake na kutoa maamuzi ya haki, ambayo yatamaliza minong'ono na hisia.

Hata hivyo, tunaona kuna umuhimu kwa NEC kuongeza uwazi zaidi hususan baada ya kushughulikia rufani zinazohusu uteuzi.

Tunasema hivyo kutokana na majina ya walioshinda pingamizi au kukataliwa kutokutajwa ili umma ukawafahamu, hivyo kuondoa kabisa mijadala na malalamiko yanayoendelea.

Pamoja na kwamba walipoweka mapingamizi hawakutajwa majina yao hadharani, lakini NEC kama chombo kinachowajibika kwa umma, kwa kuwataja itakuwa imewapa haki wananchi kuelewa ni kina nani wagombea halali wa maeneo yanayohusika.

Ni matarajio yetu kuwa kila upande ukitimiza majukumu yake kama sheria, taratibu na kanuni zinavyoelekeza, hakika uwazi utatawala na kuondoa malalamiko na hisia zisizo na msingi. Kila mmoja anapaswa kuelewa kuwa uchaguzi ni kitu kinachopita, lakini kuna maisha baada ya uchaguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wasiojisaidia chooni huchangia kuzalisha wagonjwa 500,000

Na Sabato Kasika

**LAITI** wanaojisaidia ovyo mitaani wangejua kuwa, wanachangia kusababisha wagonjwa takribani 500,000 kila mwaka, kutokana na maradhi yanayotokana na vinyesi vyao, pengine wangebadilika na kutumia choo.

Takwimu zinazotolewa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Choo Duniani, kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), zinawataja watu 432,000 kuwa wanaambukizwa magonjwa, kutokana na kusambaa ovyo kinyesi kunakochangiwa na kukosekana vyoo.

Aidha, inaelezwa kuwa takribani nusu ya watu duniani (bilioni 4.2) wanaishi bila huduma za usafi.

Takwimu za UN za Novemba mwaka jana zinataja watu milioni 673, kuwa wanaendelea kujisaidia haja kubwa kwenye maeneo ya wazi kwa kukosa vyoo, na umoja huo unasisitiza kuwa usafi ni haki ya kila mmoja.

Jamii inakumbushwa kwamba, vyoo vinaokoa maisha, kwa vile kusambaa kinyesi cha binadamu kunasababisha maradhi mengi yanayokatisha maisha ya mamilioni ya watu kila mwaka.

Huduma za vyoo zinaelezwa kuwa ni mwarobaini wa kutokomeza magonjwa yanayoenezwa na vimelea na wadudu kama nzi, hivyo kuna haja ya kupanua wigo wa huduma za usafi wa vyoo na kutomwacha yeyote nyuma.

Kwa ujumla matumizi ya vyoo, tena safi na bora yanahimizwa kutokana na ukweli kwamba, kinyesi cha binadamu kisipotupwa ovyo, jamii inakuwa hatarini.

Kinyesi kinachafua maji, chakula na udongo kupitia vijidudu vya maradhi na kusababisha kuharisha na matatizo mengine makubwa ya kiafya.

Hivyo matumizi ya vyoo huzuia vijidudu kuingia katika mazingira na kulinda afya ya jamii nzima na siyo afya pekee bali kuwa na vyoo safi na bora kunasaidia, pia ni sehemu ya faragha.

Mahitaji ya faragha, ni muhimu, ndiyo maana kumekuwapo na kampeni mbalimbali zinazolenga ujenzi wa vyoo bora na kuvitumia, hasa vyenye milango kuliko vya wazi au kujisaidia vichakani.

Miongoni mwa kampeni hizo ni ile ya kitaifa ya Nyumba ni Choo inayohamasisha jamii kujenga na kutumia vyoo bora, ambayo inaratibiwa na Wizara ya Afya.

Kupitia kampeni hiyo, kaya mbalimbali zisizokuwa na vyoo huhimizwa kujenga vyoo bora na kuvitumia, huku wananchi wakikumbushwa kuwa choo bora ni kile kinachozuia kuenea kwa kinyesi katika mazingira ya binadamu.

Aidha, kinatakiwa kuwa na sakafu inayosafishika kwa maji, kiwe na usiri, mlango pamoja na paa, ikiwa ni njia mojawapo ya kulinda faragha ya mtumiaji, kuliko ilivyo sasa kwenye baadhi ya maeneo.

Zama hizi inaelezwa kuwa bado wapo baadhi ya watu wanaojisaidia vichakani, ziwani, mabondeni na maeneo mengine badala ya kutumia vyoo, hali ambayo ni hatari kiafya.

Kwa mfano, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, amewahi kukaririwa na vyombo vya habari, akiwapa onyo watu wanaojisaidia ndani ya ziwa Victoria, kwamba watachukuliwa hatua za kisheria.

Anatoa onyo wakati kampeni za Nyumba ni Choo zinaingia mkoani mwake na kuwataka wakazi wa mkoa huo kujenga vyoo bora na kuvitumia, badala ya kujisaidia maeneo ambayo siyo rasmi.

Ukweli ni kwamba, kujisaidia haja kubwa ovyo kunasababisha magonjwa hatari kikiwamo kipindupindu, ambacho kinaenezwa kwa kula chakula au kunywa maji yenye kinyesi kibichi.

Ndipo wadau wakiwamo serikali, UNICEF wasema umefika wakati jamii kutambua umuhimu wa kutumia vyoo, kwa kuunga mkono juhudi za serikali za kampeni za mara kwa mara kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Nikumbushe jamii kwamba, kujisaidia vichakani, majini na mabondeni siyo ustarabu, hivyo ni vyema jamii kuitikia kampeni hizo na kuzifanyia kazi kwa lengo la kuboresha afya ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yaokoa mil. 44/- za korosho Kibiti

**Na Futuna Seleman,** KIBITI

OFISI ya Mkuu wa Wilaya Kibiti mkoani Pwani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilaya hiyo, imeokoa Sh. 44,054,040 za wakulima wa korosho wa vyama vya ushirika.

Vyama hivyo ni Mwambao Amcos na Ruaruke Amcos vya Wilaya ya Kibiti za mauzo ya korosho msimu wa mwaka 2019/2020.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gullam Hussein Kiffu akitoa taarifa ya kuokoa fedha za wakulima wa korosho Kibiti, alisema korosho za vyama hivyo ziliuzwa katika mnada wa Januari 24, 2020 kwa kampuni ya RV. EXPORT zikiwa jumla ya kilo 157,591 ambapo baada ya korosho kuuzwa, mnunuzi alichukua kilo 71,845 na kuacha kilo 85,746 ambapo korosho zilizobaki ziliendelea kukaa ghalani hadi TAKUKURU na ofisi ya mkuu wa wilaya ilipofuatilia suala la wakulima wasiolipwa walipwe

Aidha baada ya ufuatiliaji kuanza ilibainika kuwa mnunuzi wa korosho alikuwa ameshalipa fedha CORECU kwa ajili ya wakulima wa Mwambao na Ruaruke na baada ya fedha hizo kulipwa hazikuwafikia wakulima walengwa badala yake CORECU walizipeleka kwa wakulima wengine wasiohusika.

"Suala hili liliendelea kufuatiliwa na Ofisi ya TAKUKUKURU na Agosti 28, 2020 kikao cha pamoja ambacho kilishirikisha ofisi ya mkuu wa wilaya, TAKUKURU na ofisi ya mkurugenzi na viongozi wa AMCOS husika alisema na kuongeza:

"Tulikaa kwa pamoja na ndipo ilipoamuliwa kwamba CORECU wawalipe wakulima fedha zao ndani ya siku 14."

"Napenda kuwajulisha kuwa CORECU wametekeleza kilichoagizwa na wamelipa kiasi cha Sh. 44,054,040 ambapo mnaziona hapa na nyingine tayari tumeshawalipa wakulima," alisema mkuu wa wilaya.

Kiffu aliongeza kuwa ufuatiliaji fedha za wakulima wa korosho ulianza tangu Novemba 2019 ambapo hadi leo Sh. 300,920,780 zimeokolewa na kulipwa kwa wakulima ambao walikuwa hawana tena matumaini ya kupata fedha zao.

Alitoa wito kwa viongozi wa AMCOS na CORECU kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa ili kuepusha hujuma kwa mazao ya wakulima wanyonge ambao wanatumia gharama kubwa kwenye madawa, lakini baada ya mavuno fedha zao au mauzo yao yanahujumiwa na watu wachache.

"Lakini pia kampuni ya ununuzi wa mazao ya wakulima wa Kibiti nawaasa kuacha ujanja ujanja wa kuwadhulumu wakulima badala yake fuateni sheria, kanuni na taratibu kwani mtajikuta mnaingia katika matatizo ambayo yatayumbisha biashara, "alisema Kiffu.

Awali Kamanda wa TAKUKURU Kibiti, Anna Shine, alisema walipokea malalamiko kutoka kwa vyama viongozi wa Ruaruke Amcos na Mwambao Amcos kuwa baadhi ya wakulima wanadai fedha zao na walikwenda hadi ofisi ya mkuu wa wilaya na wao walianza kushughulikia madai hayo.

"Korosho ziliuzwa kwa kampuni ya RV ambaye alizibeba nusu nyingine akaziacha kwa madai ya changamoto ya barabara na ubovu wa korosho lakini cha kushangaza ofisi ya mkuu wa wilaya ilifanya mnada mwingine na mnunuzi huyohuyo akaja tena kuzikagua na kukubali kuzichukua ambapo wakulima walikubali wakatwe kufidia ubovu wa barabara kwa kutoa Sh. 80 kwa kila kila fedha ilizoingizwa kwenye akaunti ya CORECU lakini CORECU walichukua fedha hizo hizo na kupeleka kwa wakulima wengine ambao si walengwa, ".alisema Anna.

Hata hivyo alisema walikaa Pamoja na uongozi wa chama kikuu cha msingi Mkoa wa Pwani CORECU na Amcos jitihada zilizosaidia kubaini fedha zilipopelekwa ambazo zimerudishwa na kupewa walengwa.

Kamanda Anna aliwataka wananchi wa Kibiti waitumie vizuri ofisi yao kwani wananchi wengi wamepata haki zao kupitia ofisi hiyo.



Ofisa Taaluma wa Mkoa wa Pwani, Asnath Samwel (kushoto), akimkabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo kwa njia ya TEHAMA ya kuwajengea uwezo kutoa elimu kwa wanafunzi, kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Chole, iliyopo Kisarawe mkoani humo, Zainery Ngonyani, yaliyotolewa na shirika lisilo la kiserikali la GESCI kwa walimu wakuu na viongozi wa shule za sekondari za mkoa huo, wa Pwani, mjini Kibaha juzi. Katikati ni Meneja Mradi wa ADSI Tanzania, Joyce Msolla. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 15,000 kupata elimu ya kilimo cha mboga

**Na Renatha Msungu,** ARUSHA

KITUO cha Utafiti wa Mbegu za Mboga cha Tengeru, kinatarajia kuwafikia wananchi 15,000 kuwafundisha kilimo cha mboga na matumizi ya mbegu bora.

Mtafiti wa Kituo hicho, Alaik Laizer, alisema jana jijini Arusha kwua lengo lao ni kuona wakulima wananufaika na kilimo chenye tija.

Laizer alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi na vikundi vya wajasiriamali katika mikoa mbalimbali ili kuwainua katika kilimo hicho.

Alisema kituo hiko kimekuwa kikizunguka katika mikoa mbalimbali kuhakikisha wakulima wanalima kisasa ili kuwa na kilimo chenye tija.

"Tuna kazi kubwa ya kuwafundisha wakulima kuendesha kilimo cha kisasa cha mboga," alisema Laizer.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa wakulima katika vikundi wameamka na kuendesha kilimo cha mboga cha kisasa na kuwafundisha wenzao.

Mtafiti Ritha Luoga alisema kituo hicho kimesaidia wanawake wengi kuinuka kiuchumi kupitia kilimo cha mboga na sasa wengi wanafanya kilimo chenye tija.

Alisema lengo lao ni kuona kilimo cha mboga na matunda kinakua kwa kasi nchini.

Msimamizi wa mradi wa kilimo hicho Unguja na Pemba, Judith Assenga, alisema unaendelea vizuri, akibainisha kuwa visiwani huko, wanawashauri wakulima walime mboga aina ya mnafu na mgagani ambazo zinahitajika kwa kiasi kikubwa.

Alisema mnafu una soko kubwa visiwani huko kwa sababu unahitajika kwa wingi na wanaolima ni wachache.

Alisema moja ya vikwazo ambavyo wakulima wanakutana navyo ni kutokufahamu aina za mboga zinazofaa kulimwa katika maeneo ambayo wanalima mboga.

# World Vision yatia mkono vita malaria

**Na Happy Severine,** ITILIMA

KATIKA kuhakikisha ugonjwa wa malaria unatokomezwa, Shirika la World Vision Tanzania limetoa vyandarua 6,160 vyenye viuatilifu kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi.

Vyandarua hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 38.6 vimetolewa kwa watoto wafadhiliwa 3,431 na wengine 2,729 wasiofadhiliwa kupitia mradi wa malaria wa shirika hilo.

Mratibu wa Mradi wa World Vision, Nyamoko George, alibainisha hayo jana wakati wa ugawaji wa vyandarua hivyo, uliofanyika katika ofisi za shirika hilo, Kanadi wilayani Itilima.

George alisema wanatambua kuwa malaria ni moja ya magonjwa yanayoongoza kwa kusababisha vifo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na kushuka kwa kiwango cha mahudhurio shuleni pindi wanapougua ugonjwa huo mara kwa mara.

"Watoto wengi wenye miaka chini ya mitano wanaugua malaria na kupoteza maisha na wengine huugua malaria mara kwa mara hali inayowafanya kutohudhuria vyema masomo shuleni," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema shirika linaungana na serikali katika kupambana na kutokomeza ugonjwa huo huku wakiamini vyandarua walivyovitoa vitasaidia kupunguza kama si kuisha kabisa malaria kutoka asilimia saba hadi chini ya asilimia moja ifikapo mwishoni mwa mwaka huu pamoja na kutokomeza kabisa (zero malaria) ifikapo mwaka 2030.

Akitoa taarifa ya hali halisi ya ugongwa huo wilayani Itilima, Mganga Mfawishi wa Hospitali ya Wilaya, Anorld Musiba, alisema malaria bado ni ugonjwa unaowasumbua sana wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017 hadi 2019, bado tatizo ni kubwa, hivyo jitihada za dhati zinahitajika katika kuutokomeza.

"Mwaka 2017 kulikuwa na wagonjwa wa nje (OPD) 9,764 kati ya hao 4,159 sawa na 43 walikuwa watoto chini ya miaka mitano. Mwaka 2018 walikuwa 6,209 kati ya hao 2,460 sawa na asilimia 40 walikuwa watoto chini ya miaka mitano na mwaka jana walikuwa 6,432 kati yao asilimia 41 walikuwa watoto chini ya miaka mitano.

"Mwaka huu, kuanzia Januari hadi Julai, walikuwa 3,088 ambapo watoto walikuwa 1,449 sawa na asilimia 46.9," alisema.

Awali, akipokea vyandarua hivyo, Katibu Tawala wa Wilaya, Philbert Kanyilizu, aliwaomba wadau mbalimbali wajitokeze kushirikiana na serikali kutokomeza ugonjwa huo.



Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Jacqueline Maleko (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa chama hicho, Mwajuma Hamza (kushoto) na Mjumbe wa Bodi, Mery Sila, wakizindua tuzo za wanawake waliofanya vizuri zaidi kwa mwaka 2020 katika sekta ya viwanda na biashara jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tuzo wanawake waliofanya vizuri kibiashara yazinduliwa

**Na Frank Monyo**

CHAMA cha Wanawake wenye Viwanda na Biashara (TWCC) kimezindua tuzo za wanawake waliofanya vizuri zaidi mwaka 2020 katika sekta za viwanda na biashara nchini.

Tuzo hizo zinatarajiwa kutolewa Novemba 28, 2020 jijini Dar es Salaam na kuambatana na uzinduzi wa Jarida la Wanawake 100 Wajasiriamali waliothubutu (Tanzania Inspire & Impact Women Book), kitachotumika kutangaza kazi mbalimbali za wanawake wajasiriamali nchini.

Mwenyekiti wa TWCC, Jacquiline Maleko, akizungumza na jijini Dar es Salaam jana, alisema usajili kwa ajili ya tuzo hizo ni bure na zitawahusu wanawake wote wajasiriamali hata ambao sio wanachama wa TWCC.

Alisema tuzo hizo zinalenga kuonyesha mchango wa mwanamke mjasiriamali katika kukuza uchumi wa nchi na kuchochea maendelo ya jamii.

"Tuzo hizo zina lengo la kutambua na kuheshimu wanawake waliofanikiwa na wale wanaochipukia katika sekta za viwanda na biashara, kujenga imani juu ya ujasiriamali na kuhamasisha wanawake wa vizazi vijavyo kuwekeza na kujishughulisha katika shughuli za viwanda na biashara pamoja na kusherehekea mafanikio wanayoyapata wanawake katika sekta za viwanda na biashara," alisema Maleko.

Aliongeza kuwa wanawake ni nguzo muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote, na kwamba wanawake wana uwezo wa kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya viwanda na biashara endapo wataaminiwa na kupewa nafasi yakufanya hivyo.

Aidha, Maleko aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya biashara, ambapo wanawake wengi wameweza kuanzisha biashara na viwanda vidogo ambavyo vimewaongezea kipato, kuzalisha ajira pamoja kuchangia katika kukua kwa uchumi wa nchi.

Alisema kuwa mchakato wa upatikanaji wa washindi wa tuzo hizo unaratibiwa na kamati maalum inayoundwa na wajumbe kutoka taasisi za serikali na sekta binafsi.

"Ili kuweza kushiriki katika tuzo hizi wanawake wanatakiwa kujaza fomu maalum ambazo kwa sasa zinapatikana bure katika tovuti ya TWCC www.twcc-tz.org, ofisi za serikali za mikoa, halmashauri, ofisi za TWCC mikoa mbalimbali, SIDO na ofisi zote za TCCIA," alisema Maleko.

# Viongozi dini Marekani, Rwanda kuombea corona

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

VIONGOZI wa dini kutoka nchi za Marekani na Rwanda wameahidi kuombea nchi zao na zingine kuondokana na janga la ugonjwa wa corona kupitia ardhi ya Tanzania.

Wamesema hiyo inatokana na Tanzania kuwa nchi pekee duniani ambayo watu wake wanaendelea na kazi zao kama kawaida licha ya kuwapo na tishio la ugonjwa huo duniani.

Viongozi hao akiwamo Mchungaji kutoka Kanisa la Waamini la nchini Marekani, Dana Morey, walisema hayo jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari juu ya kuanza kwa semina ya dini Manispaa ya Morogoro.

Mchungaji Morey alisema Tanzania ni nchi ambayo watu kutoka mataifa mbalimbali wanaiongelea kwa sababu ya kuwa na utulivu na watu wanatembea kwa uhuru nyakati hizi za corona kutokana na maombi ya siku tatu yaliyoongozwa na Rais John Magufuli ya kuondoa ugonjwa huo.

Alisema nchi zingine zinaendelea kusumbuka na virusi vya corona na Tanzania imepata jibu ambalo ni kumfanya Mungu kuwa kimbilio.

"Tanzania mnaonyesha ni namna gani mnamjua Mungu, hakuna kiongozi aliyeweza haya kutoka nchi zingine, lakini Tanzania imetumia siku tatu kwa kusali na Mungu akakubali maombi yenu," alisema Mchungaji Morey kutoka Marekani.

Alisema wameamua kuja Morogoro kama sehemu yao ya kwanza kutembelea Tanzania kutangaza neno la Mungu baada ya kuingia ugonjwa wa corona, huku wakija na neno moja kwa wanadamu kuwa wamwamini Mungu kwa maana yeye anawapenda na ndio maana akamtoa mwanaye wa pekee afe msalabani ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.

Mchungaji Morey alisema kupitia maombi yanayoanza leo hadi Jumapili watakaoshiriki watabadilisha maisha yao ikiwamo kuondoshwa kwa magonjwa yaliyowasumbua kwa muda mrefu yatakwisha.

Naye Muinjilisti kutoka kanisa la Mwanga wa Mataifa la nchini Rwanda, Dk. Lau Tumusime, alisema Tanzania ndio nchi pekee ambayo inakubali mikutano na mikusanyiko na wananchi wanaitika kuomba.

Alisema wameamua kutumia mwaka 2020/21 kuja Tanzania baada ya Mungu kuwaelekeza kutoa huduma nchini humo.

Naye Mwenyekiti wa makanisa ya Pentekoste (TAG) mkoani Morogoro, Askofu Bryson Msuya, alisema katika semina hiyo pia watamwomba Mungu aivushe salama Tanzania katika kipindi cha uchaguzi, kupitia maombi ya amani na umoja yatakayoendelea wakati wa semina hiyo.

# Waafiki kushtakiwa wachafuzi wa kelele

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU kadhaa baada ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) litangaze azima yake ya kuwashtaki wachafuzi wa kelele na mitetemo, wananchi wamepongeza hatua hiyo.

"Hatua ya kuwaburuza mahakamani wachafuzi wa kelele na mitetemo ni ya kupongezwa na kila Mtanzania kwani hali ni mbaya. Kelele zinawakosesha watu utulivu na kukosekana kwa ufanisi wa shughuli zao," alisema Muhsin Lingai, mkazi wa Vingunguti jijini Dar es Salaam.

Daud Machuma mkazi wa eneo la Viwanda Mikocheni jijini Dar es Salaam alisema kuwashtaki wakaidi kutaleta amani wakati wa usiku wakati viwanda vingi vinakuwa vinaendelea na uzalishaji.

"Mikocheni ni eneo la viwanda. Tunavipenda viwanda kwa sababu vimeajiri vijana wetu. Lakini lazima sheria ya mazingira iheshimiwe ili kupunguza athari hasi kutoka viwandani. Kupunguza kelele za usiku ni busara kubadilisha teknolojia," alisema.

Alex Mushi, mkazi wa Sinza, alilitaka baraza kutomwogopa mtu yeyote katika kusimamia sheria na kanuni za mazingira.

"Kuna kelele nyingi katika makazi ya watu kutoka vyanzo mbalimbali. Hasa Sinza kelele zinatoka kwenye kumbi za starehe na baa. Tunaipongeza NEMC kwa kutamka kwamba itachukua hatua kwa mujibu wa sheria. Na wafanye hivyo, bila kujali rangi, kabila wala dini ili kuleta utulivu katika makazi ya watu," alisema Mushi.

Alidai kuwa wamiliki wa baa na kumbi za starehe walio wengi hawajali mahitaji ya watu wengine zaidi ya kuwafurahisha wateja wao jambo linawanyima watu wengine nafasi na haki ya kutulia na familia katika makazi yao.

"Kwenye makazi yetu tuna wagonjwa, watoto wadogo, wazee, wafanyakazi na watu tunaohangaika mchana kutwa katika harakati za kulijenga Taifa. Tunaporejea kwenye makazi yetu tunahitaji utulivu na mapumziko ya muda mrefu. Lakini hali imekuwa tofauti kwa kuwa tunakaribishwa na kelele na kelele zinaendelea kwa usiku kucha," alisema.

Hivi karibu Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka, alisema kuwa NEMC haitasita kuwaburuza mahakamani wakiukaji wa sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na katika kusimamia hilo hawatomwonea mtu na pia hawatampendelea yeyote kwa rangi yake, dini, kabila au cheo chake.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Uendeshaji na Teknohama wa Benki ya Maendeleo, George Wandwalo (kulia), pamoja na baadhi ya wafanyakazi wenzake wakichangia damu, katika maadhimisho ya miaka saba ya utoaji huduma wa benki hiyo, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaoishi kando ya reli kuwezeshwa

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limewakutanisha wadau kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi kujadili juu ya njia bora za kuwawezesha wananchi wanaoishi kando kando ya reli kunufaika na fursa zilizopo katika reli.

Wakizungumza wakati wa mkutano huo uliofanyika hivi karibuni Ihumwa jijini Dodoma, wadau hao waliipongeza serikali kupitia TRC kwa kutekeleza mradi huo, huku wakisisitiza umuhimu wa wananchi wanaoishi kandokando ya miradi ya reli kuhakikisha wananufaika na fursa zinazotokana na miradi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema lengo la kuwakutanisha wadau hao ni kujadili na kutoa maoni yao namna mradi huo unavyopaswa kutekelezwa kwa kuzingatia mahitaji yote muhimu kwa wananchi wanaouzunguka.

Kadogosa alisema mradi huo pamoja na mambo mengine, unasaidia kuchagiza maendeleo katika maeneo yanayouzunguka kwa kuwa unahusisha pia uboreshaji wa huduma za jamii ikiwamo za afya na miradi ya wananchi kujiongezea kipato.

Dk. Edwin Lyala, mtaalamu wa Ikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema mkutano huo ni muhimu kwani ulisaidia kutoa nafasi kwa washiriki kujadili na kubadilishana mawazo juu ya masuala mbalimbali ikiwamo fursa za kiuchumi na uhifadhi wa mazingira katika miradi ya reli.

Dk. Lyala alisema ipo haja ya kulinda urithi wa asili, jadi, mila pamoja na masilahi ya wakulima na wafugaji katika kipindi chote cha utekelezaji wa miradi hiyo ya reli. "Tunapaswa kuhakikisha kuwa wale waliohamishwa kutoka kwenye mradi wanapewa ardhi kuendeleza maisha yao," alisema Dk. Lyala.

Catherine Masao, mhadhiri na mtafiti kutoka UDSM, alisema kuna haja ya kuanzisha kozi za uhandisi wa reli ili kutoa wataalamu zaidi wa kuhudumu katika sekta hiyo kwa kuwa bado inaonekana kuwa na upungufu wa wataalamu.

# Balozi wa heshima Seychelles aipongeza Tanzania sheria afya

**Na Frank Monyo**

BALOZI wa heshima wa Seychelles nchini, Maryvonne Pool, ameipongeza Tanzania kwa hatua iliyofikia katika usimamizi wa sheria ya afya na usalama mahali pa kazi yenye lengo la kulinda nguvu kazi ya Taifa.

Balozi Pool, amesema anatambua kazi nzuri inayofanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 na kupitia sheria hiyo maeneo mengi ya kazi yanatambulika na kuzingatia viwango vya usalama na afya kazini.

Kauli hiyo ameitoa jana jijini Dar es Salaam alipotembelea ofisi za OSHA kwa lengo kufanya usajili wa moja ya miradi ambayo ofisi yake ni mbia pamoja na kujifunza namna ambavyo taasisi hiyo inavyotekeleza.

"Naipongeza Tanzania chini ya uongozi wa Rais John Magufuli kwa kuwa na taasisi muhimu kama hii ambayo inasaidia kulinda nguvu kazi ya nchi na nimekuwa nikiwasikia sana siku hizi na nafahamu jinsi mlivyojipanga katika kutekeleza majukumu yenu ya msingi," alisema Balozi Pool.

Akiwa katika ofisi hizo ameahidi kushirikiana na OSHA katika kuviwezesha vikundi vya wakulima wadogo wanaofanya shughuli zao katika wilaya za pembezoni mwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuhakikisha vikundi hivyo vinasajiliwa na OSHA kwa ajili ya kujikinga na madhara yatokanayo na shughuli za kilimo.

"Sisi tunafanya miradi mbalimbali ya kuwawezesha wakulima kuboresha uzalishaji na kupata masoko ya mazao ya kilimo na japokuwa tumekuwa tukiwawezesha wakulima kupata vifaa muhimu vya kujikinga kama viatu vya shambani, lakini tunaona ipo haja ya kuwahamasisha wakulima kuwa katika vikundi vya uzalishaji na kuwawezesha kupata usajili wa OSHA, ili mwendelee kuwaongoza kufanya kazi zao kwa usalama zaidi," alisema Balozi Pool.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema taasisi yake imefarijika kutembua kwamba juhudi za serikali za kulinda nguvukazi ya Taifa zinaonekana.

"Tumefurahi sana leo kutembelewa na Balozi wa heshima wa Seychelles nchini kwetu ambaye amekuja kusajili eneo lake la kazi. Tumepata fursa ya kushirikishina mambo mengi na kubadilishana uzoefu jinsi ambavyo nchi zetu zinasimamia masuala ya afya na usalama ambapo amefurahi sana kuona kwamba nchi yetu ina mfumo madhubuti wa kusimamia usalama na afya ili kulinda nguvu kazi ya Taifa," alisema Mwenda.

# Wateja wa Tigo sasa wapata fursa mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, imezindua huduma mpya ambayo inampa mteja uwezo wa kurefusha muda wa matumizi ya kifurushi ambacho kinakaribia kufikia ukomo wa muda wake wa matumizi.

Huduma hii mpya itawapa wateja fursa na uwezo wa kuendelea kutumia kiasi cha kifurushi kilichobakia baada ya kufikia kikomo cha muda awali wa matumizi.

Hii itahusisha vifurushi vya kupiga simu, kutuma meseji pamoja na data.

Huduma hii ya kuweza kurefusha muda wa matumizi kwa kifurushi kilichofikia kikomo cha muda wake wa matumizi maarufu kama 'Chukua Kilicho Chako' ni ya kwanza na ya aina yake na kampuni ya Tigo ndiyo ya kwanza inayompa uhakika mteja kuwa sasa hataweza kupoteza kifurushi chake ambacho hakijatumika.

Meneja wa kitengo cha bidhaa za intaneti, Ndevonaeli Eliakimu, alisema: "Kama mtandao wa kisasa wa mawasiliano nchini, tumewasikiliza na tumeamua kufanyia kazi ombi hilo la wateja wetu ambao wamekuwa wakishindwa kutumia vifurushi vyao kutokana na kuisha kwa muda wake wa matumizi. Hivyo basi huduma hii mpya itawapa wateja uwezo wa kuongeza au kurefusha muda wa matumizi wa vifurushi vyao kuanzia siku, wiki hata mwezi".

"Kama kampuni ya mawasiliano inayoongoza kwa kutoa huduma za kidigitali na za kisasa kabisa nchini Tanzania, tumekuwa wa kwanza kuzindua huduma hii mpya na ya aina yake, hivyo wateja wetu sasa hawatakuwa na wasiwasi juu ya ukomo wa muda wa matumizi wa vifurushi vyao. Huduma hii inazidi kudhihirisha namna Tigo inavyojidhatiti kuhakikisha inawathamini wateja wake kwa kuwapatia huduma zenye ubunifu wa hali ya juu," Eliakimu ameongeza.

"Hivyo basi kwa sasa vifurushi vitakuwa vinatumika kulingana na matakwa ya mteja na hii pia inadhihirisha ushindi kwa wateja wote wa Tigo nchini Tanzania na ni matumaini yetu kwamba huu ni mwendelezo wa kuboresha huduma zetu, ili kumrahisishia mteja wetu namna ya kuwasiliana na wapendwa wake," alisema Eliakimu.

# Serikali yaahidi utatuzi kero usafirishaji bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, amewaahidi wasafirishaji bidhaa nje ya nchi kuwa serikali itashughulikia mapendekezo na changamoto wanazokumbana nazo ili wafanye biashara kwa ufanisi.

Prof. Shemdoe aliyasema hayo jana katika kikao kilichowakutanisha wadau wa usafirishaji bidhaa nje na watendaji wa serikali.

"Serikali inatambua changamoto mnazokutana nazo. Nasema wazi kuwa haya mliyoyapendekeza ninayachukua na ninawaahidi kuyapeleka sehemu husika na yatapatiwa ufumbuzi," alisema Prof. Shemdoe.

Prof. Shemdoe aliwaomba wasafirishaji bidhaa nje ambao ni wanachama wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kuandaa vikao vya majadiliano walau mara nne kwa mwaka.

"Naomba muwe mnaandaa vikao hivi walau mara nne kwa mwaka. Vikao hivi vitatupa dira sahihi ya kujua wapi tunakwenda na wapi tunakwama ili pafanyiwe marekebisho," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Zachy Mbenna, alimshukuru Prof. Shemdoe kwa kushiriki kwake katika kikao na kueleza kuwa TPSF inaridhishwa na uhusiano kati yake na serikali. "Kwa namna ya pekee naipongeza sana serikali kwa namna wanavyoshirikiana na sisi na niseme wazi kuwa sisi tuko nyuma ya serikali kuhakikisha uchumi wa nchi yetu unazidi kuimarika," alisema Mbenna.

Mbenna aliwataka wasafirishaji wa bidhaa nje wajitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa zilizopo ndani na nje ili kuiingiza fedha za kigeni.

"Nchi yetu inaingiza fedha nyingi za kigeni kupitia sekta hii ya usafirishaji bidhaa nje ya nchi, sasa nitoe rai tu kwa wadau mujitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa hii ili serikali ipate mapato na wasafirishaji wapate mapato," alisema Mbenna.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, alisifu ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi, na kuiomba serikali kuzibadilisha sera na sheria zinazokwamisha usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

"Ni wazi serikali ya Rais John Magufuli, inajitoa sana kushirikiana na sekta binafsi... hili ni jambo la kuvutia sana kwani maendeleo ya nchi yoyote muhimu kuhusisha sekta binafsi," alisema Kirenga na kuongeza: "Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na serikali, ombi langu kubwa sasa ni hizi sera na sheria zinazotukwamisha sekta hii zipitiwe na zifanyiwe maboresho ili tuweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi."

## Wizara yafafanua madai utoaji mitaji biashara bila riba

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema taarifa zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii kuwa inashirikiana na Shirika binafsi la BACC kutoa mitaji ya biashara na kilimo bila riba wala vikwazo siyo za kweli.

Akizungumza jijini Dodoma, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, alisema taarifa hiyo ipuuzwe kwa kuwa wizara inautaratibu maalumu wa kufikisha taarifa kwa umma.

"Wizara hutumia njia rasmi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii iliyosajiliwa na kutambulika na serikali kutoa taarifa zake, hivyo ni vema kutambua kuwa wizara haihusiki katika taarifa hizo zenye lengo la kupotosha umma na kuibua sintofahamu miongoni mwa jamii," alisema Mwaipaja.

Aliitaka jamii kujihadhari na genge hilo la matapeli wanaotumia mitandao ya kijamii kuwarubuni ili kujipatia fedha za wizi.

Alisema kuwa wizara haitambui na wala haijawahi kujihusisha kwa namna yoyote na kampuni hiyo na wala wizara haina mradi wowote wa namna hiyo wa kuwakopesha wafanyabiashara na wakulima mikopo isiyo na riba wala vikwazo.

"Hao ni matapeli wa kimtandao, wapuuzeni," alisisitiza Mwaipaja.

Aidha, aliwaonya watu wanaofanya vitendo hivyo kuacha mara moja kwani wanatafutwa na vyombo vya dola kwa udi na uvumba na kwamba wakipatikana hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mwaipaja aliwataka wote ambao watapenda kupata maelezo ya ziada kuwasiliana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Namba ya simu namba 075481562.




Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dk. Bernard Kibesse (kulia), akimpongeza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, baada ya kuzindua kadi za NMB Prepaid na Credit, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yazindua kadi za kisasa za malipo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB kwa kushirikiana na kampuni ya Mastercard imezindua matumizi ya kadi za kisasa zaidi za kielektroniki ambazo zinatarajiwa kuwa chachu ya mapinduzi makubwa ya malipo nchini na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa watu wengi

Kadi hizo zinazowezesha malipo ya kabla (prepaid card) na malipo kwa mkopo (credit card) zilizinduliwa rasmi jijini Dar es Salaam Jumatatu katika hafla iliyoshuhudiwa na wadau mbalimbali akiwamo Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse.

Kwa mujibu wa viongozi wa benki hiyo, ushirikiano na Mastercard kutoa huduma hizi mbili utakuwa wa manufaa mengi na mafanikio makubwa si kwa wateja wa NMB tu bali pia kwa sekta ya kifedha na Watanzania wote.

Dk. Kibesse alisema litakuwa jambo jema kama lengo hilo litakuwa maradufu ili huduma hii mpya iweze kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwapo na uhakika wa Watanzania wengi kuwa na huduma za kibenki muda wote na mahali popote.

Alisisitiza umuhimu wa kadi hizo kusambazwa hadi vijijini na maeneo ya pembezoni kwa kuwa faida yake ni pamoja na kuwasaidia wakulima kujiwekea akiba hata kabla ya kufungua akaunti.

"Sekta ya benki leo tena inashuhudia mapinduzi makubwa hususani katika kuhakikisha kuwa Taifa la Tanzania linapiga hatua katika matumizi ya kadi na kutupeleka katika nyanja za kimataifa," alisema Dk. Kibesse.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema huduma ya kadi za malipo ya kabla na zile za malipo kwa mkopo ni moja ya miradi mikubwa ambayo taasisi hiyo imefanya na Mastercard. Mwaka 2015, washirika hao wawili walizindua Mastercard debit cards ambazo zimesambazwa kwa wateja zaidi ya milioni tatu.

Mradi wa pili ulikuwa ni uzinduzi wa Mastaboda ambayo inawawezesha waendesha pikipiki kupokea malipo kupitia simu za mkononi. Zaipuna alisema mradi huu mpya na wa tatu na Mastercard ni ushirikiano wa muhimu sana na wa faida kwa sekta ya fedha nchini na kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi, alisema uzinduzi wake unathibitisha utayari wa NMB kupanua wigo wa kuwawezesha Watanzania kuingia katika mifumo ya malipo ya kidijitali yaliyo salama na rahisi zaidi.

Akizungumza kwa njia ya video kutoka Nairobi, Kenya, Mkurugenzi Mkazi wa Uendelezaji Biashara wa Kampuni ya Mastercard Afrika Mashariki, Frank Molla, alisema ubia wa kampuni hiyo na NMB ni sehemu ya mkakati wao wa kuwafikia watu bilioni moja duniani na kuwaingiza kwenye uchumi wa kidijitali mpaka ifikapo mwaka 2025.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 10, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kijiji kinapojenga ofisi'kali' kuliko DC, DED**



Ukurasa 13

'Majiko sanifu ya umeme ndiyo mwokozi pekee misitu'



Ukurasa 14

**UNICEF bega kwa bega upatikanaji, usambazaji chanjo ya COVID-19**

AFYA

Na Sabato Kasika

# NI BALAA SIGARA

## •Inazichoma 30,000/- za mvutaji 'deile'
## •Muhimbili yaitaja magonjwa ya moyo

IWAPO unavuta sigara jifahamu kuwa unatumia wastani wa takriban Sh. 28,840 kwa mwezi. Fedha hizo si haba. Kwa mujibu wa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, kwa mvutaji angeweza kuzitumia kuondoa umaskini kwenye familia.

Waziri anasema matumizi hayo makubwa ya tumbaku kwa mtu mmoja yangetumika kupunguza umaskini wa chakula kwa mwanafamilia mmoja kwa asilimia 85, lakini fedha hiyo inachomwa na kuteketezwa licha ya kwamba tumbaku inatajwa kuwa na madhara kiafya.

Waziri anasema hayo wakati akipokea ripoti ya utafiti wa matumizi ya tumbaku ya wateja wenye zaidi ya miaka 15 uliofanyikwa mwaka 2018.

"Kutokana na takwimu hizo, ni wajibu wa wizara kuendelea kutoa elimu na kupanua wigo kuhusu madhara, ili kama mtu anaamua kuvuta, awe anafahamu madhara makubwa yanayoweza kumtokea," anasema.

Kwa kutumia matokeo ya viashiria muhimu vya utafiti wa mapato na mtumizi ya kaya kwa mwaka 2017 hadi 2018, pesa za kujikimu kwa ajili ya mahitaji ya msingi kwa mwezi kwa mtu mmoja ni Sh. 49, 320, na mahitaji ya chakula kwa mwezi ni Sh. 33, 748.

**UVUTAJI NCHINI**

Waziri Ummy anasema, utafiti uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa kukusanya viashiria kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini sera ya mipango endelevu ya maendeleo, yaliyoanishwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo 2016/17-2020/21 unaonyesha kuwa wanaovuta tumbaku ni milioni 2.6.

"Kwa ujumla matokeo hayo yanaonyesha Tanzania haipishani na nchi nyingine barani Afrika kati ya mwaka 2012 hadi 2018 ikiwamo Kenya na Cameroon, kwani wavutaji wapo chini ya asilimia 12," anasema.



Dk. Lutgardi Kagaruki, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF). **PICHA: MTANDAO**

Waziri anawaagiza watendaji wa wizara yake kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia upya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku ili iendane na Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Tumbaku.

**KILIO CHA WADAU**

Dokta Lutgard Kagaruki, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF), ambaye anaiomba serikali izuie janga la tumbaku na kupitisha haraka sheria ya kuidhibiti.

Kagaruki anasema inahitajika ili iendane na mkataba wa kimataifa unaokataza matumizi ya kilevi hicho.

"Hilo ndilo ombi letu la miaka yote na tunaendelea kuliwasilisha zaidi ili kusaidia vijana wasijiingize katika uvutaji mapema kabla hawajatambua madhara ya tumbaku," Dk. Kagaruki anasema.

Anaongeza kuwa tumbaku ni kisababishi kikubwa cha magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo saratani, matatizo ya moyo, kisukari na mengine sugu hasa ya kifua na huua takribani watu 8,000,000 kwa mwaka duniani.

"Kati ya hao, zaidi ya 7,000,000 ni wavutaji, huku milioni 1.2 ni wasiovuta bali wanaovutishwa moshi wa tumbaku. Na kwa Tanzania, tumbaku huua watu 14,700 kwa mwaka, ambayo ni asilimia nne ya vifo vyote," anasema.

Anasema, utafiti uliofanywa na TTCF ikishirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mwaka 2009, pale ORCI na MNH, ilionekana kuwa, asilimia 32 ya saratani zote zilihusishwa na matumizi ya tumbaku.

Dk. Kagaruki anaongeza kuwa, katika mwaka huo, serikali ilitumia dola milioni 40 (karibu bilioni 100) kujaribu kutibu saratani hizo.

Wakati hayo yakitokea tumbaku ilikuwa imeeliingizia taifa dola milioni 50 (karibu sawa na Sh. bilioni 115) kwa mwaka huo.

"Mwaka 2014, utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Muhimbili matokeo yalionyesha kuwa Tanzania ilitumia dola milioni 136, kujaribu kutibu magonjwa ya moyo yaliyosababishwa na matumizi ya tumbaku," anasema.

Matibabu hayo ni kwa wale waliofika hospitalini na ukweli ni kwamba wapo wengi ambao hawakutafuta

Anafafanua kuwa mwaka 2019, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, ilielezwa kwamba, kuzibua mshipa mmoja ulioziba kutokana na utumiaji tumbaku uligharimu dola 13,000 (takriban Sh. milioni 30).

"Ukweli ni kwamba, biashara ya tumbaku huleta vifo na hasara nyingi zaidi, kuliko faida kidogo sana inayoingia kwenye pato la serikali," anasema.

**SHERIA ZINASEMAJE?**

Sheria ya matumizi ya tumbaku inapinga 'promosheni' ya sigara, inataka matangazo yote yaambatane na ujumbe kama "sigara inamwathiri jirani yako; uvutaji sigara unaua; matumizi ya tumbaku yanaua.

Inasema, uvutaji wa sigara unaweza kusababisha saratani, unaleta magonjwa ya mapafu. Na pia inataka bidhaa zote za tumbaku ndani na nje ya nchi ziwe na kiwango cha ubora wa Shirika la Viwango la Taifa (TBS) na kukataza watu wenye umri chini ya miaka 18 kutumia au kuvuta bidhaa za tumbaku.

Mtu anayebainika akivunja sheria hiyo, anaweza kupigwa faini ambayo si chini ya Sh.5,000,000 na si zaidi ya milioni 20 au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu au adhabu zote kwa pamoja

Pia katika makosa mengine mtu anaweza akatozwa faini ya Sh. 2,000,000 au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela.

MAZINGIRA

# Kijiji kinapojenga ofisi'kali' kuliko DC, DED

## •Chajivunia mabilioni hifadhi ya misitu



Sehemu ya ofisi za Kijiji cha Mihima iliyojengwa kwa kutumia rasilimali za misitu. **PICHA:BEATRICE PHILLEMON.**

**Na Beatrice Philemon, LINDI**

WANAKIJIJI cha Mihima wanaoishI Kata ya Namupa wilayani Lindi ni 'wajanja' tena wana kila sababu ya kufurahi baada ya serikali kuutangaza msitu wao kuwa ni hifadhi.

Hatua hiyo inawapa nguvu na mamlaka ya kisheria, serikali ya kijiji na wananchi kusimamia na kuhifadhi msitu huo, kupasua mbao, kukata magogo kwa ajili ya miradi maendeleo ya kijiji.

Mihima ni moja ya vijiji tisa ambavyo misitu yake yenye ukubwa wa hekta 27,000 imetangazwa na serikali kuwa ya hifadhi na vijiji vina hati miliki.

Mingine ni ya vijiji vya Kiwawa, Ruhoma, Milola Magharibi, Kinyope, Likwaya Muungano, Mkombamisi na Makumba.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaib Ndemanga, anasema hayo alipokabidhi Tangazo la Serikali namba 487 la Juni 2020 la Sheria ya Misitu kwa Mwenyekiti wa Mihima, Maimuna Swalehe, kumjulisha kuwa msitu huo ni hifadhi.

"Tangazo Namba 487 la mwaka 2020, linataja Msitu wa Mihima kuwa umehifadhiwa kisheria. Kupitia shughuli za usimamizi shirikishi wa Misitu na uhifadhi wa misitu, kijiji cha Mihima kina uwezo wa kufanya shughuli za maendeleo, "Nawapongeza kwa kazi nzuri mliyofanya hadi kufikia hatua hii ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali," anasema Ndemanga.

**MAFANIKIO**

Usimamizi shirikishi wa msitu kijijini Mihima unaelezwa na Mwenyekiti Maimuna Swalehe kuwa umeleta manufaa makubwa kutokana na kuuza mbao na magogo na kutumia fedha na kujenga miradi ya maendeleo kijijini.

> **"Nasema pia baada ya kuvuna misitu kijiji kilinunua pikipiki kwa ajili ya kwenda msituni kufanya doria..." anaongeza Mwenyekiti wa Kijiji.**

Wamefanikiwa baada ya kufuzwa na masuala mengi kama utawala bora na uhifadhi wa misitu yaliyotolewa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA),Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mpingo Conservation and Development Initiatives, (MCDI) na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili (TFCG).

Anasema mafunzo hayo yameifanya Mihima kuwa kijiji pekee wilayani Lindi kuwa na matumizi endelevu ya mapato ya kijiji kwa kujenga ofisi ya kisasa bora kuliko za Mkuu wa Wilaya ya Lindi na Mkurugenzi wa Halmashauri.

"Haya ndiyo tunayotaka kuona. Mapato ya rasilimali za misitu yafanye kazi inayoonekana, lazima matunda ya fedha hizo yaonekane." Anasema Ndemanga.

Aidha, kijiji kimejenga madarasa mawili, choo chenye matundu nane Shule ya Msingi Mihima,ofisi ya walimu mkuu, nyumba ya mwalimu, kutengeneza barabara yenye kilomita 14 na kuweka kifusi na kujenga daraja.

"Ninaomba wanavijiji wengine waje Mihima kujifunza jinsi mlivyoweza kufikia hatua hii" anasema Ndemanga.

Mbali na hilo Wilaya ya Lindi, inataka misitu10 mingine ya vijiji ikifika mwaka 2022 itangazwe na itambulike kisheria na wananchi wanufaike na rasilimali zake.

"Hatutaki msitu uwe shamba la bibi, au mtu aingie kuvuna mazao yetu, lazima misitu ipimwe, iwe na matumizi bora ya misitu na pia tuvune misitu kadri ya mpango mzuri wa uvunaji na uhifadhi wa misitu ili msitu wetu utusaidie leo, kesho na vizazi vijavyo," anasema

Mbali na hilo, Ndemanga anawaomba viongozi wa Mihima kuendelea kusimamia mapato yote ya kijiji yanayotokana na mazao ya misitu kama mbao, magogo na mengine.

"Mtumie vizuri fedha hizo na hakikisheni wananchi wote wanajua, msiamue kitu bila kushirikisha wananchi, uamuzi wote unayohusu misitu lazima washirikishwe wananchi. Nasema hivi kwa sababu sehemu yoyote ambayo fedha inaingia kunaleta migogoro," anasema.

Mbali na hilo, anawaomba Ofisa Misitu wa Wilaya kuendelea kutoa elimu kwa kamati za maliasili na wananchi ili waendelee kusimamia matumizi bora na pia kuwatembelea ili kuona matatizo yanayowakabili katika shughuli za usimamizi na uhifadhi wa msitu .

Pia wananchi au walinzi wakifanya vizuri muwape motisha,"kulinda msitu siyo kazi nzuri ni hatari kuna wanyama, tembo, nyati majangili, kama wakipewa motisha,wananchi msione kuwa watu hawa wanapendwa sana au wanapendelewa.

Mhasibu wa Kamati ya Maliasili Kijiji cha Mihima, Malunda Liloko, anasema wamefarijika na msitu kutangazwa na serikali kuwa msitu wa hifadhi ya kijiji.

Anasema msitu huo una ukubwa wa hekta 3,125 na wakazi wa Mihima 2,258, wanaume ni 1,073 na wanawake 1,185 na kaya ni 311.

"Kupitia uhifadhi wa msitu tumepata mafanikio makubwa lakini bado tunahitahi elimu ya usimamizi shirikishi wa misitu yetu na jinsi ya kupima vipimo au ujazo wa mbao tunazovuna," ana Liloko.

"2018, kijiji kilivuna mbao zenye ujazo wa mita 500 zenye thamani ya Sh. milioni 91.4, mwaka 2019 kilivuna pia mbao zenye zenye thamani ya Sh. milioni 110 na mwaka huu 2020 tumevuna zenye thamani milioni 70 zilizotumika kutekeleza miradi ya maendeleo ya kijiji."

Kabla ya kuhifadhiwa msitu huo ulikuwa na hali mbaya kutokana na uvunaji holela wa misitu kukata mbao, magogo na uharibifu kwa asilimia 90 wanatoka vijiji jirani kama Mnacho, Namang'ale, Namupa, Londo, Ndawa,

**CHANGAMOTO**

Kamati ya maliasili na serikali ya kijiji kukosa elimu ya mpango kazi, "Tukishapata fedha bado hatujui jinsi ya kutumia fedha hizo kwa sababu kila mara viongozi wanabadilishwa badilishwa angalau wangekuwa wanakaa miaka mitatu katika uongozi," anasema Liloko

Anasema wanahitaji elimu hiyo ili kuandaa mipango ya muda mrefu ya matumizi ya fedha za serikali ya kijiji.

"Wajumbe wa kamati kubadilishwa mara kwa mara kunachangia tatizo hili, ichukue miaka mitatu angalau," anaomba.

Akizungumzia mipango mhasibu huyo anasema wanatarajia kuvuta maji katika kijiji chao kwa sababu wakati wa kiangazi kunakuwa na uhaba.

"Mara nyingi wakati wa kipindi cha kiangazi tunapata maji kutoka mto Mihima kwa matumizi ya kila siku na siyo maji salama kwa matumizi ya binadamu ila tunatumia kwa sababu ya ukosefu wa maji," anasema.

Mwenyekiti wa kijiji, Maimuna Swalehe, anaomba vijiji vingine wilayani Lindi viige mfano na kujifunza usimamizi shirikishi wa misitu na kuvuna misitu yao kwa uratatibu bora.

"Kutokana na uhifadhi wa misitu, hali ya ukataji misitu holela holela imepungua, msitu wetu umeimarika na wanyama kama nyati, swala na matunda ya aina mbalimbali yaliyokuwa yametoweka lakini sasa yamerudi, na watu wanayavuna," kwa mujibu wa Maimuna.

Anasema wananchi wanaendelea kufanya doria kwenye msitu ili kutoa taarifa serikali ya kijiji na wajumbe wa kamati ya maliasili kuhakikisha msitu unakuwa salama.

"Nisema pia baada ya kuvuna misitu kijiji kilinunua pikipiki kwa ajili ya kwenda msituni kufanya doria..." anaongeza Mwenyekiti wa Kijiji.

Seleboni Mushi, Ofisa Misitu wa Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii, anasema serikali itahakikisha uhifadhi wa misitu unaendelea na misitu inasimamiwa ipasavyo,

"Pia tutatoa mwongozo msitu huu uhifadhiweje, tozo, na uvunaji ufanyikeje kwa kushirikisha jamii ," anasema Mushi.

Mbali na hilo, pia halmashauri ina jukumu la kutoa elimu ya uvunaji, utawala bora, majukumu ya kamati, uhifadhi wa msitu ili kila mtu ajue anafanya nini .

Anawakumbusha viongozi wa vijiji lazima wahakikishe wanasimamia mapato kikamilifu na makusanyo wanayopata na kuwapo mpango wa matumizi bora ya fedha za mazao ya misitu.

Mbali na hilo, wizara imeandaa mpango wa usimamizi wa misitu na sheria ndogo ili wananchi waweze kusimamia msitu kwa mujibu wa sheria.

MAZINGRA

# 'Majiko sanifu ya umeme ndiyo mwokozi pekee misitu'

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na changamoto nyingi za kimazingira kama mabadiliko ya tabianchi, serikali na wadau wa mazingira jukumu lililo mbele yao ni kuwekeza na kuhamasisha matumizi ya nishati za kisasa kama jiko sanifu la umeme yenye presha.

Kuna haja ya kufanya jitihada hizo kwa vile kupika kubakia kuwa hitaji muhimu na la msingi kwa kila mmoja anayehitaji kula.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kuendeleza Huduma za Nishati Endelevu (TaTEDO), Estomiah Sawe, katika mahojiano na Nipashe, anasema zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wanategemea kuni na mkaa kupika.

Akinukuu ripoti ya mwaka huu ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaonyesha kuwa asilimia 63.5 za kaya zote nchini hupikia kuni na ndiyo nishati kuu, nyingine ni mkaa asilimia 26.2 asilimia 5.1 hupikia gesi (LPG) wakati iliyobakia 3.0 hupika na umeme.

Sawe anasema asilimia kubwa ya kuni na mkaa huwashwa kwenye majiko yasiyo sanifu kama la mafiga matatu lenye ufanisi wa chini ya asilimia 10 linatumiwa na zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa vijijini.

Aidha, mijini kaya nyingi hutumia majiko ya mabati ya mkaa yasiyo na ufanisi mengi yako chini ya asilimia 15. Matumizi haya ya kuni na mkaa yanachangia sana katika uharibifu wa mazingira na maisha, anaongeza.

"Ni chanzo cha uharibifu na kutoweka misitu. Hapa nchini, zaidi ya hekta 469,871 za misitu ya asili hutoweka kila mwaka." Anasema Sawe.

**UMEME NCHINI**

Anasema uzalishaji wa umeme umewafikia wananchi kwa asilimia 78.4, ingawa wateja wanaotumia wadogo kwenye asilimia 37.7 na katika kaya nyingi unatumiwa zaidi kwa mwanga, kuchaji simu, redio, TV na matumizi mengine madogo.

"Hata hivyo kaya zenye umeme zinaendelea kununua nishati nyingine kama gesi, mkaa na kuni kupikia. Gharama huwafanya watu kuchagua nishati ya kutumia. Kama teknolojia zinazotumika kwenye nishati fulani zinaleta unafuu na rahisi zaidi inakuwa na wateja wengi zaidi... Umeme unapatikana, hauagizwi nje kama gesi (LPG), hauharibu mazingira kama kuni na mkaa, uko safi, watu wengi wanashindwa kuutumia kwa sababu teknolojia ya jiko la kawaida la umeme inatumia mwingi. Kwa hiyo kinachokwamisha ni gharama." Anasema mtaalamu huyo.

"Kubadilisha teknolojia na nishati ni kipaumbele hasa taifa linapoingia uchumi wa kati na ni mkakati muhimu wa kuliwezesha kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN) na ya nishati endelevu kwa wote ifikapo mwaka 2030.". Anasema .



Wapishi wakifurahia jiko sanifu la umeme lenye presha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

**CHANGAMOTO ZINAZOKWAMISHA**

Wadau wa teknolojia wanaozungumza na gazeti hili wanasema pamoja na faida nyingi zitokanazo na kupika kwa nishati za kisasa ikiwemo afya, mazingira na uchumi, bado hapajakuwepo mafanikio ya kutumia kwa wingi nishati na teknolojia za kisasa za kupikia. Hali hii inatokana na sababu kadhaa, upande wa sera, upande wa wafanyabiashara na watumiaji. Sera na mikakati ya kuendeleza nishati na teknolojia za kupika hazijapewa kipaumbele wala uwekezaji wa kutosha .

Baadhi ya nishati za kupikia zinaagizwa nje, na hutozwa kodi ya zaidi ya asilimia 40 ya bei ya kununulia na kuzifanya ghali ambazo wananchi hushindwa kuzimudu.

Teknolojia ya majiko sanifu ya umeme yenye presha (JULEP) haijajulikana, lakini ni nafuu kuliko nyingine zote tatizo ni olojia ni gharama ya kununulia jiko hilo ambayo inatokana na kodi kubwa zaidi ya asilimia 46, ya ongezeko la thamani asilimia 18, wanayotozwa mwingizaji na msambazaji pamoja na ushuru wa kuagiza nje wa asilimia 10

Wadau hawa wanapongeza juhudi zinazofanywa na serikali kufikisha umeme kwenye kaya nyinyi lakini zinaendelea kutumia kuni na mkaa kutokana na unafuu na kukosa ufahamu wa nishati nyingine.

**UDHAIFU SERA, TAASISI**

Wakichambua sera na taasisi wadau wa nishati za kisasa za kupikia, wanasema hajakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji yanayotarajiwa. Mara nyingi juhudi nyingi za kufanikisha miradi ya kuwafikishia wananchi umeme kwa ajili ya kuwasha taa na matumizi mengine zimeendelea kufanyika na kusahau kuendeleza nishati ya kupikia.

Hivyo kuwaacha wengi wategemee kuni na mkaa kwa njia zisizo na ufanisi. Waathirika wakubwa ni wanawake na watoto, hasa wasichana wanaotafuta kuni za kupikia.

Hapajakuwepo mikakati na program za kitaifa za kutatua hali hiyo kutokana na kukosa kipaumbele kwenye sera, mikakati na bajeti ya nishati kwa ajili ya kupikia, wanasema wadau.

**HALI YA SOKO**

Uchambuzi wa soko la nishati na teknolojia za kupikia hapa nchini, unaonyesha kuwa soko rasmi la nishati ya kupikia halijaendelezwa na limebakia kutegemea kuni na mkaa. Serikali imejiwekea lengo la muda mrefu la kuhakikisha zaidi ya asilimia 75 ya kaya nchini zinatumia nishati na teknolojia za kisasa kupikia ifikapo mwaka 2030.

Nishati na teknolojia zinazopewa msukumo, zinajumuisha, gesi (LPG), gesi ya samadi (bayogesi), umeme na majiko sanifu. Lakini juhudi zinazofanyika hazijaleta matokeo ya kuridhisha.

Aidha, juhudi za kuendeleza bayogesi hazijawafikia wananchi wengi kutokana na gharama za awali za kutengeneza miundombinu kuwa kubwa na changamoto ya kuihudumia kila siku.

Majiko ya umeme yanuzwa kwa gharama kubwa, umeme pia ni ghali yote hayo yanawafanya wasipikie umeme. Kwa majiko sanifu, juhudi chache zimefanyika kukuza matumizi yake kwenye kuni na mkaa, lakini kutokana na bajeti na uwekezaji mdogo kwa wajasiriamali na watumiaji, mafanikio si ya kuridhisha.

Pamoja na juhudi zote za kukuza matumizi ya majiko sanifu ya kuni na mkaa si endelevu na hazijawa za muda mrefu. Kutegemea kuni na mkaa kutaendelea kutokana na ongezeko la watu ambalo linaweka mzigo mkubwa kwenye misitu.

Gesi ya mitungi au LPG inatokana nje na usafishwaji wa siyo endelevu kwa kipindi cha muda mrefu. Pamoja na kuwa siyo endelevu, pia inaweza kuwa siyo ya kuaminika kutokana na kuwa inaagizwa kutoka nje na inategemea soko la mafuta ambalo Tanzania haiwezi kulidhibiti, bei na hata upatikanaji wake, hivyo kuwa na uwezekano wa watumiaji kurudia kuni na mkaa inapokosekana bei ikipanda.

Hivyo gesi nayo inakuwa nishati ya mpito na ukweli siyo suluhisho la kudumu, Tanzania inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza gesi kutoka nje.

Licha ya kuwa na gesi asilia na juhudi zinaendelea kukuza matumizi yake kama ilivyo LPG siyo endelevu kwa kuwa baada ya muda itamalizika lakini pia kwa kiwango inachangia kuongezeka hewa ya ukaa.

Pia miundombinu ya kuwezesha kutumika nyumbani ni ya gharama kubwa, hivyo kusababisha wachache kufikiwa na nishati hiyo.

Lakini pia inawezekana kupoteza kuitumia gesi asilia kuzalisha bidhaa za thamani kubwa zaidi ikiwa itatumiwa kupikia.

Hivyo upo umuhimu wa serikali kutafuta na kutumia nishati na teknolojia ambayo ni endelevu na nafuu kwa ulinzi wa afya, mazingira na kupunguza gharama.

AFYA

# UNICEF bega kwa bega upatikanaji, usambazaji chanjo ya COVID-19

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), limetangaza kufanya kazi kwa karibu na kampuni wazalishaji dawa na washirika wengine kufanikisha kupatikana chanjo ya virusi vya corona au COVID-19, kuzisafirisha na kuzihifadhikwa niaba ya kituo cha kimataifa cha corona cha COVAX.

Aidha, imetangaza kuongoza juhudi hizo za upatikanaji na usambazaji wa chanjo ya COVID -19 katika operesheni kubwa zaidi duniani na ya haraka ya upatikanaji na usambazaji wa chanjo kama sehemu ya mpango wa kimataifa wa chanjo wa COVAX unaosimwamiwa na Muungano wa Chanjo Duniani (GAVI).

Wakati aina mbalimbali za chanjo zikionyesha matumaini, UNICEF kwa kushirikiana na Shirika la Afya La Amerika (PAHO) wataongoza juhudi hizo ili kupata chanjo kwa ajili ya nchi 92 za kipato cha chini na zile zinazoelekea kipato cha wastani ambazo ununuzi wa chanjo zake utapigwa jeki na mkakati maalum wa GAVI -COVAX.

Lakini pia UNICEF itakuwa mratibu wa upatikanaji wa chanjo hiyo pia kwa ajili ya nchi 80 za kipato cha juu ambazo zimeonyesha dhamira ya kushiriki mchakato wa COVAX na zitagharamia chanjo hizo kwa kutumia bajeti binafsi.

Wengine watakaoshirikiana na UNICEF kufanikisha kazi hiyo ni Shirika la Afya Duniani (WHO), (GAVI), Umoja wa Kugundua, Kukabili na Kuhimili, Magonjwa ya Milipuko (CEPI), PAHO, Benki ya Dunia, Wakfu wa Bill na Melinda Gates na wadau wengine.

Kituo cha COVAX kiko tayari kushirikiana na nchi zote ili kuhakikisha kuwa hakuna nchi itakayoachwa nyuma bila kupata fursa ya chanjo ya COVID-19 itakapopatikana ili kudhibiti ugonjwa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF, Henrietta Fore, anasema "Huu ni ushirika wa nguvu baina ya serikali, kampuni ya utengenezaji wa dawa na wadau wengine mbalimbali wa kuendeleza vita dhidi ya janga la COVID-19. Ni nia yetu ya pamoja ya kusaka chanjo, UNICEF inatumia uwezo wake wa kipekee katika usambazaji wa chanjo kuhakikisha kwamba nchi zote zina fursa salama ya haraka na iliyo sawa katika kupata chanjo za awali punde zitakapopatikana."

Shirika hilo ndilo mnunuzi mkubwa zaidi wa chanjo duniani ambapo kila mwaka hununua zaidi ya dozi bilioni mbili za dawa hizo kwa ajili ya kampeni za kawaida za chanjo na kukabiliana na milipuko ya magonjwa mbalimbali kwa niaba ya karibu nchi 100 duniani.

Lakini pia ni mdau mkubwa wa shirika hilo ni GAVI ambayo kwa zaidi ya miaka 20 UNICEF imeweza kuwafikia zaidi ya watoto milioni 760 na chanjo za kuokoa maisha na hivyo kuzuia zaidi ya vifo milioni 13.

UNICEF itatumia utaalam wake kusaka masoko kuratibu upatikanaji na usambazaji wa chanjo za COVID-19 kwa ajili ya kituo cha COVAX.




Wafanyakazi wa UNICEF wakipakua dawa mbalimbali. **PICHA :UN NEWS.**

**KITISHO CHA HEWA CHAFU**

Wakati huohuo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, ameonya kuwa wakati umefika wa kushikamana na kuchukua hatua zinazohitajika dhidi ya hewa chafu inayovutwa na watu tisa kati ya 10 kila siku duniani kote.

Kupitia ujumbe wake wa maadhimisho ya kwanza ya siku ya kimataifa ya hewa safi kwa ajili ya anga ya bluu, Guterres anaonya kwamba hewa chafu inayovutwa inachangia kwa kiasi kikubwa magonjwa ya moyo, kiharusi, saratani ya mapafu na maradhi mengine ya mfumo wa hewa.

Anaongeza kuwa "Inasababisha takriban vifo milioni 7 visivyo vya lazima kila mwaka hususan katika nchi za kipato cha chini na cha wastani. Uchafuzi wa hewa pia unatishia uchumi, uhakika wa chakula na mazingira."

Taarifa hiyo ya Katibu Mkuu imesema wakati huu ambapo dunia inajikwamua kutoka kwenye janga la corona inapaswa kutoa msukumo mkubwa kuhusu suala la uchafuzi wa hewa ambao pia unaongeza hatari zinazohusiana na COVID-19.

Anasisitiza kwamba: "Ni lazima pia tushughulikie haraka tishio kubwa la mabadiliko ya tabianchi, kuhakikisha ongezeko la joto duniani linasalia nyuzi joto 1.5 hali ambayo itasaidia kupunguza uchafuzi wa hewa, vifo na magonjwa."

Akitoa mfano anasema mwaka huu hatua za kudhibiti kusambaa kwa corona zilizolazimisha kufungwa kila kitu na watu kusalia nyumbani zimesaidia kiwango cha kuchafua hewa kushuka kwa kiasi kikubwa na hivyo kutoa matumaini ya hewa safi katika miji mingi.

Hata hivyo, anaonya kwamba uchafuzi wa hewa tayari unaongezeka tena na katika baadhi ya maeneo zaidi hata ilivyokuwa kabla ya COVID-19, hivyo "Kuliko wakati mwingine wowote sasa tunahitaji mabadilio makubwa na ya kimakati . Kusisitiza hatua za viwango vya mazingira, sera na sheria ambazo zinazuia wachafuzi wa hewa."

Guterres anazitaka nchi pia kuacha kutoa ruzuku kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya visukuku (fossils) mfano petroli.Katika ngazi ya kimataifa na kuzitaka kushirikiana

ili kusaidiana kuingia katika teknolojia za hewa safi.

Anatoa wito kwa serikali mbazo bado zinafadhili miradi ya mafuta ya kisukuku katika nchi zinazoendelea kuelekeza ufadhili huo kwenye nishati safi na usafiri endelevu.

Aidha, anazitaka nchi zote kutumia fungu la kujikwamua baada ya COVID-19 kusaidia kuunga mkono mabadiliko ya kuingia katika ajira zenye afya na endelevu.

Siku ya kimataifa ya hewa safi kwa ajili ya anga ya bluu itaendelea kuadhimishwa kila mwaka Septemba 7, kuanzia mwaka huu na katika maadhimisho haya ya kwanza Katibu Mkuu Guterres ametaka ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya kujenga mustakabali wenye hewa safi kwa wote.

***UN NEWS***



Vyanzo vya uchafuzi wa hewa kama hivi vinavyotishia afya duniani **.PICHA: MTANDAO.**



# TARI yatafiti mbegu mpya za zabibu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Makutupora, iko katika hatua za mwisho kukamilisha utafiti wa aina tano za mbegu za zabibu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini.

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Cornel Massawe, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu utafiti huo na mikakati ya kupanua uzalishaji wa zao hilo nchini.

Alisema kituo hicho kimeelekeza nguvu katika kuendesha utafiti zaidi katika zabibu, ili kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima unakuwa na tija.

"Tunavyosema mbegu bora ni zile zenye vigezo na zinazotakiwa na mkulima na zina tija ya kutosha, zinahimili mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame au mafuriko na magonjwa," alisema.

Dk. Massawe alisema aina hizo zinazofanyiwa utafiti, mbili ni kwa ajili ya kutengenezea mvinyo, mbili na moja kwa ajili ya viungo.

Alibainisha kuwa kwa sasa Tanzania kuna aina mbili za mbegu ya zabibu ambazo zimefikishwa kwa wakulima na zote ni za kutengeneza mvinyo. "Katika jitihada za kupanua wigo wa mbegu nchini tumeshirikiana na wenzetu wa Afrika Kusini ambao wametupatia aina 13 za mbegu ambazo zote ni kwa ajili ya mvinyo na ziko kwenye mafungu mawili nyeupe na nyekundu," aliongeza.

Mkurugenzi huyo alisema lengo lao baada ya mbegu hizo kufika nchini wataziweka kwenye kituo cha utafiti na kuangalia zile ambazo zimeweza kuhimili hali ya hewa ya Tanzania na kupelekwa kwenye maeneo yanayolima zabibu nchini.

"Tunavyochukulia kwa sasa maeneo yanayolima zabibu kwa wingi nchini ni wilaya za Bahi, Dodoma na Chamwino. Hata hivyo, tafiti (utafiti) zilizofanyika (uliofanyika) zinaonyesha (unaonyesha) zabibu inaweza kustawi katika ameneo mengi ya Tanzania kuanzia Ruvuma, Mara, Tabora, Kilimanjaro, Tanga na Singida," alisema.

Hata hivyo, alisema hatua hiyo inawapa matumaini kwamba hiyo mikoa italima zabibu kwa kiwango cha juu.

"Mkakati tulionao kwenye hizi mbegu zilizopo nchini ambazo tumefanyia utafiti kwa sasa zipatikane kwa kiasi cha kutosha kukidhi mahitaji. "Tumeingia kwenye mpango wa kuhakikisha tunapanua wigo wa mbegu nchini," alisema.

Hivi karibuni, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akikabidhi matrekta kwa TARI kwa ajili ya kuongeza uzalishaji mbegu wa mazao mbalimbali nchini, alisema serikali imeamua zao hilo kuwa moja ya mazao ya kimkakati.

"Mahitaji ya zabibu kwa sasa ni makubwa kutokana na ujenzi wa viwanda vya kuchakata mvinyo na matumizi mengine mengi. Kama nchi tumejipanga kuhakikisha hili zao tunaliendeleza, kuwekeza vya kutosha na kuzalisha kwa kiwango kikubwa ili kukidhi mahitaji ndani ya nchi na nje," alisema.

Hasunga alisema ujenzi wa viwanda vya zabibu utachangia kuwapo na ajira nyingi na kuchangia uchumi wa nchi kwa kuongeza thamani.



Mratibu wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme Tanzania, Kenya na Zambia mkoani Dodoma, Mhandisi Peter Kyadje (aliyenyoosha mkono), akitoa maelezo kwa wakurugenzi wa mradi wa umeme wa vijijini (REA), walipotembelea kwa ajili ya kukagua upanuzi unaoendelea wa ujenzi wa kituo cha Zuzu, Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mapato ya ndani Jiji la Dodoma yafikia bil. 52/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeongeza ukusanyaji mapato ya ndani kutoka Sh. bilioni 3.6 kwa mwaka 2015/16, hadi Sh. bilioni 52.1 kwa mwaka 2019/20.

Akizungumza na Nipashe kuhusu ukusanyaji mapato, Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema ongezeko hilo la makusanyo ni sawa na asilimia 788.

Alisema makisio ya jiji hilo kwenye makusanyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 4.5 kwa mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 59.1 sawa na ongezeko la asilimia 1,298. Pamoja na makisio hayo, alisema kiasi kilichokusanywa ni Sh. bilioni 3.6 sawa na asilimia 80.

"Kwa mwaka 2016/17, makisio yalikuwa Sh. bilioni 3.9 na zilikusanywa Sh. bilioni 4.8 sawa na asilimia 123," alisema.

Mafuru alisema kwa mwaka 2017/18, makisio yalikuwa Sh. bilioni 20.7, lakini zilikusanywa Sh. bilioni 25.03 sawa na asilimia 121 huku mwaka 2018/19, makisio yalikuwa Sh. bilioni 71.9 na zilikusanywa Sh. bilioni 58.2 sawa na asilimia 87.

"Mwaka 2019/20, tuliweka makisio ya kukusanya Sh. bilioni 59.1 na hadi Juni, mwaka huu, tumekusanya Sh. bilioni 52.1 sawa na asilimia 88," alisema.

Kuhusu hoja za ukaguzi, Mafuru alisema Jiji limepunguza hoja za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutoka 161 kwa mwaka 2015/16 hadi 46 kwa mwaka 2018/19 sawa na asilimia 71 ya punguzo.

"Pia Jiji kwa miaka mitatu mfululizo limefanya vizuri katika ukaguzi uliofanywa na CAG kwa kupata hati safi yenye msisitizo mpaka kufikia 2018/19 tofauti na mwaka 2015/16 ambapo ilipata hati yenye mashaka," alisema.

# Wachinjaji, wenye bucha watakiwa kuzingatia usafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa machinjio ya kuku na wamiliki wa bucha za nyama katika Jiji la Dodoma, wametakiwa kuzingatia usafi ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao baada ya kukagua hali ya machinjio na bucha kwenye masoko mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

Alisema kanuni za afya zinapaswa kuzingatiwa kwenye maeneo hayo kwa kuhakikisha yanakuwa safi muda wote.

"Baadhi ya machinjio ya kuku na bucha mazingira yake si rafiki hususan katika suala zima la usafi, hivyo ni muhimu mkachukua tahadhari zote ili kutokumbwa na magonjwa ya mlipuko," alisema.

Yuna pia alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya wafanyabiashara wadogo kutozingatia usafi kwenye maeneo ambayo wanafanyia biashara zao na kusababisha taka kusambaa ovyo.

Aliwataka wafanyabiashara hao kufuata kanuni na sheria za Jiji kwa kutofanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

"Kuna tatizo wamachinga wamekuwa wakipanga bidhaa zao kwenye maeneo yasiyo rafiki wengi wanakimbilia kupanga bidhaa kando kando ya barabara ambayo inatumika kupita magari na pikipiki, hii inaweza kusababisha ajali pia na uharibifu wa bidhaa zao na hata kwa maisha yao," alisema.

Aliongeza: "Pamoja na kuwa na vitambulisho siyo sababu ya kukaidi maelekezo ambayo yapo kwa faida yenu, kinachotakiwa hapa ni kuheshimu na kuepukana na tabia ya kupanga bidhaa kwenye maeneo hatari."

Alisema kuwa Jiji halitakuwa tayari kuwaona baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka maelekezo yaliyotolewa katika kufanya biashara.





# Ajinadi kujenga barabara km70

**Na Grace Mwakalinga,** MAKETE

MGOMBEA ubunge Jimbo la Makete kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ahadi Mtweve, amewahakikishia wananchi endapo atachaguliwa, atahakikisha anajenga barabara yenye urefu wa kilomita 70 kwa kiwango cha lami kutoka katika Kata ya Chimala mkoani Mbeya hadi kwenye Hifadhi ya Kitulo.

Alisema hayo juzi katika mkutano wa kampeni huku akisema suala la barabara atalipa kipaumbele ili kutatua kero wanayoipata wananchi wanaosafiri kutoka mkoani Mbeya hadi Wilaya ya Makete.

Alisema tayari ameandaa mkakati mahususi wa namna ya kuomba fedha bungeni, ili kukamilisha ahadi hiyo katika namna ya kipekee ambayo hakuna mbunge yeyote amewahi kufanya hivyo.

"Nina mkakati wa peke yangu wa kuhakikisha tunapata barabara kutoka Chimala hadi Kituo ambayo katika kipindi changu cha miaka mitano tutaweza kuijenga kwa kiwango cha lami naomba wananchi muliandike hilo," alisema Mtweve.

Alisema katika kilomita hizo ni chache na kwamba serikali inao uwezo wa kuzijenga hivyo akipewa ridhaa ya ubunge jimboni hapo atahakikisha anasimamia utekelezaji wa ujenzi katika barabara hiyo.

"Miaka mitano iliyopita serikali iliahidi kujenga barabara hiyo na kwamba hadi sasa haijajengwa, naombeni mnipe nafasi ya ubunge ili niweze kulisimamia hili suala mwaka huu ni wa kuchagua fursa," aliongeza Mtweve.

Alisema yeye na wenzake walianzisha mkakati wa kudai halmashauri ndani ya Jimbo la Makete baada ya kuona wananchi hutumia umbali mrefu kwenye kufuata huduma za kiserikali hali inayosababisha wakazi hao kuamua kujiandikisha kama wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Mbarali.

Alidai endapo atapata ridhaa ya kuwa mbunge wa jimbo hilo, atatoa Sh. milioni 10 kwa kila kata kwa ajili ya kuwasaidia vijana kupata mitaji ili kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ambacho kwa sasa kinatija.

# Mgombea aahidi kujenga shule kila mtaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MGOMBEA udiwani wa kata ya Itezi, jijini Mbeya, Sambwee Shitambala, amesema endapo atachaguliwa na wananchi kuwa diwani atahakikisha kila mtaa unakuwa na shule ya msingi na kwamba suala hilo atalisimamia kwa nguvu zake zote.

Shitambala aliyazungumza hayo juzi wakati wa ufunguzi wa kampeni zake ambazo zilifanyika viwanja vya Shule ya Msingi Gombe. Alisema kwa sasa kuna idadi kubwa ya watoto na shule zilizopo hazikidhi mahitaji, hivyo kuna haja ya kujenga shule za msingi katika kila mtaa, ili kuhudumia watoto wote ambao wamefikia umri wa kwenda shuleni.

Licha ya kuahidi kusimamia ujenzi huo, alisema ili kufanikiwa lazima wananchi wajitolee nguvu kazi na baadaye serikali itaweka mkono wake kukamilisha.

"Elimu ni moja ya masuala ambayo yamejipambanua vizuri kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Endapo nitapata ridhaa ya kuwaongoza nawaahidi nitalisimamia vyema suala hili kwa sababu mimi ni mdau mkubwa wa maendeleo. Niliwahi kujenga vyumba viwili vya madarasa kwenye Shule ya Msingi Tambuka Reli," alisema Shitambala.

Aliongeza kuwa ili hayo yatimie ni lazima wananchi watambue na kumchagua kiongozi ambaye atawaletea maendeleo kwa kuhakikisha anawasilisha mahitaji yao kwenye vikao vya Baraza la Madiwani. Alisema kata hiyo pia ina shule moja ya sekondari ambayo kimsingi haitoshi kuwahudumiwa wanafunzi wote wanaofaulu, hivyo alisema kuna haja ya kujenga shule nyingine ili kukidhi mahitaji ya watoto wanaofaulu darasa la saba sambamba na kuhamasisha ujenzi wa hosteli kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike na kusoma kwa utulivu ili kutimiza malengo yao.

Naye mgombea ubunge Mbeya Mjini kwa tiketi ya CCM, Dk. Tulia Ackson, aliwataka wananchi wa jimbo hilo kutokubali kufanya maandamano ya aina yoyote kwa mashinikizo yanayotolewa na baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani kwa lengo la kuchafua amani ya nchi.

Na badala yake wasikilize na kuchambua sera za wagombea mbalimbali ili kutambua ni kiongozi gani ambaye atawaletea maendeleo na sio kiongozi anayehamasisha vurugu na maandamano.



Mgombea ubunge kwa tiketi ya CCM Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimnadi mgombea udiwani Kata ya Itezi, Sambee Shitambala, wakati wa ufunguzi wa kampeni za diwani huyo, zilizofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Gombe juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Polisi yaanzisha kampeni kupunguza ajali bodaboda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIKOSI cha usalama barabarani kimeanzisha kampeni maalum ya kupunguza ajali za bajaji na bodaboda kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu hasa mijini inayofahamika kwa jina la "Darasa Kijiwe" ambalo litasimamiwa na askari wa usalama barabarani wakiwa kama walezi.

Kazi kubwa ya Darasa Kijiwe itakuwa kutoa elimu kwa vijana wanaoendesha pikipiki za matairi matatu (bajaji) kuzingatia sheria za usalama barabarani na watumiaji wengine wa barabara ikiwamo magari na watembea kwa miguu.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Fortunatus Musilimu, alitangaza kuanza kwa Darasa Kijiwe akiwa mkoani Mbeya kwenye ziara ya kikazi.

Alisema kampeni hiyo inatokana na malalamiko ya baadhi ya madereva wa magari ya abiria na malori ya masafa marefu jijini Mbeya kuhusu usumbufu wanaoupata kutoka kwa madereva wa bajaj ikilinganishwa na bodaboda.

"Kampeni hii ya darasa kijiwe itakuwa na askari wa kikosi cha usalama barabarani kutoa elimu kwa vikundi vya bodaboda, bajaji na wananchi kwenye maeneo mbalimbali ya mikusanyiko juu ya namna ya kepukana na ajali kwa kuhakikisha waheshimu sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani," alisema Musilimu.

Alisema kampeni hiyo ambayo itafanyika nchi nzima itaongeza uelewa juu ya masuala ya usalama barabarani kwa abiria na watumiaji wa vyombo vya moto katika kukabiliana na ajali.

Licha ya kueleza mikakati ya kampeni hiyo ya darasa kijiwe alisema kiwango cha ajali za matukio makubwa kimepungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma na kwamba inatokana na madereva kutii sheria za usalama barabarani bila shurti kutokana na elimu inayoendelea kutolewa.

Alisema licha ya matukio ya ajali kupungua bado kuna baadhi ya madereva hawafuati sheria na ikitokea wamepigwa faini huishia kulilalamikia Jeshi la Polisi na kuhisi kuonewa.

Miongoni mwa madereva ambao walipata nafasi ya kusikiliza maelezo ya Kamanda Musilimu akiwa katika ukaguzi eneo la mteremko wa Iwambi, Hassan Rashid, alisema kero kubwa inayowasumbua ni madereva bajaji kutokuzingatia sheria za usalama barabarani.

Alisema madereva bajaji wengi wanaendesha ovyo kwenye barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) hali ambayo inaweza kusababisha ajali licha kudai wanajitahidi sana kuwakwepa.

Aliliomba Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani



# Maalim Seif aahidi mfumo mpya wa uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema iwapo atateuliwa kuwa rais wa Zanzibar, atahakikisha anaweka mfumo mpya wa uongozi ambao utajali na kuwaheshimu wananchi kwa mujibu wa katiba.

Alisema mfumo huo mpya utaongoza serikali kwa kuzigatia haki na fursa sawa kwa wananchi wote bila ya kujali itikadi ya kisiasa.

Hayo aliyaeleza katika kongamano la vijana wa Chama cha ACT-Wazalendo ambalo limeandaliwa ngome ya vijana ya chama hicho na kuwashirikisha vijana kutoka mikoa yote ya Unguja. Alisema mfumo huo utakaoongoza nchi, utaheshimu na kuzingatia haki zote za binadamu, ambapo kila mwananchi atapata fursa na haki sawa bila ya kujali dini na itikadi ya siasa.

"Waheshimiwa, Mungu akijalia mkanichagua nitahakikisha kwamba tunaweka mfumo mpya wa uongozi, huku kila Mzanzibar anufaike na kushi vizuri," alisema Maalim Seif.

Pia alisema kwamba serikali inayokusudia kuiunda endapo atachaguliwa, atahakikisha inazingatia msingi yote ya utu pamoja na kulinda serikali ya Zanzibar.

Maalim Seif ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho taifa, alisema kwamba atahakikisha anaibadilisha Zanzibar na kuifanya ya kuwa mfano wa kuingwa ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Malengo yangu ni kuweka misingi ambayo itakwenda kuibadilit Zanzibar kuwa mfano wa kuigwa ndani ya Afrika," alisema.

Kwa upande wao vijana katika kongamano hilo walimwomba Maalim Seif endapo atachaguliwa asiwasahau, na kuhakikisha anatatua kero ya ajira bila ya kubagua kwa misingi ya itikadi za watu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa msimamizi wa ujenzi wa nyumba za Kwahani unaofanywa na kampuni ya Estim Construction, Emanuel William (wa pili kulia), alipokuwa akikagua maendeleo ya mradi huo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ`**

# SMZ yafagilia uwekezaji kiwandani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameipongeza Kampuni ya Uwekezaji ya Basra Textile Milles kwa kazi kubwa ya kukifufua upya kiwanda cha nguo cha Cotex kilichopo Mtaa wa Chumbuni.

Amesema hatua hiyo inakwenda sambamba na azma ya serikali ya kuimaisha sekta ya kiwanda nchini.

Akiwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya uimarishaji wa miundombinu ya kiwanda hicho inayotarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu kwa awamu ya kwanza, Balozi Seif alisema hiyo ni kazi nzuri ambayo faida itakayopatikana itasaidia sio kwa wawekezaji bali kwa Taifa na vijana katika suala la ajira.

Alisema kiwanda cha Cotex kwa miaka mingi kimekuwa eneo la magofu lililokuwa likilalamikiwa na wananchi kwa kutoendelezwa licha ya serikali kumpa mwekezaji aliyeshindwa kukiendeleza kwa zaidi ya miaka 25 iliyopita.

Balozi Seif alisema nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayosaidia kutoa ajira kwa kundi kubwa la vijana na kuongeza mapato ya Taifa.

Aliushauri uongozi wa kampuni kujitahidi kuzalisha bidhaa zenye kukidhi viwango vya masoko ya kitaifa na kimataifa.

Aliuhakikishia uongozi huo kwamba Serikali ya Zanzibar iko tayari kuendelea kutoa msukumo, ili kuona malengo ya kuanzishwa mradi huo kwa vile yanawagusa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Ahmed Osman, alisema harakati zinazoendelea hivi sasa ni ufungwaji wa mashine ili kukamilisha awamu ya kwanza.

Osman alisema majaribio ya kwanza ya uzalishaji wa kiwanda hicho yanatarajiwa kuanza rasmi Oktoba mwaka huu kwa hatua za uzalishaji wa vitenge, vitambaa vya sare za shule na mashuka.

Alisema hatua hiyo ya awamu ya kwanza itawezesha bidhaa zitakazozalishwa mbali ya kutumika nchini, pia mpango umeshatayarishwa wa nyingine kuuzwa katika mataifa ya magharibi mwa Afrika.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Basra Textile Milles, Said Hassan, alisema awamu ya kwanza iliyogharimu Dola za Kimarekani milioni 21.3 itawezesha kutoa ajira 454 za wafanyakazi na awamu ya pili wafanyakazi 1,200.

Said alisema awamu ya tatu itakayotoa ajira 1,600 itakwenda sambamba na ununuzi wa zao la pamba kutoka Tanzania Bara ili kuimarisha uwezo wa wakulima wazalendo.

Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia, aliuhakikishia uongozi wa kiwanda hicho kwamba serikali itazipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza wakati wa ukarabati.

Alisema kiwandi hicho kilichoanza kuwa tegemeo kubwa la ajira kwa kundi la vijana, ni eneo muhimu litakaloleta faida kwa wananchi wa visiwa vya Zanzibar.

## Corona yakwamisha ujenzi wa nyumba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MARADHI ya corona yamesababisha ucheleweshaji wa ujenzi wa nyumba mpya za makazi zinazojengwa na Serikali ya Zanzibar zilizopo Mtaa wa Kwahani Mjini Zanzibar.

Ujenzi huyo ulitarajiwa kukamilika mwazoni mwa mwezi huu, lakini kutokana na ugonjwa huo ulioikumba Tanzania, ujenzi huo utakamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Akitoa taarifa ya mradi wa ujenzi wa nyumba hizo za Kwahani kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alipofanya ziara katika ujenzi huo, mshauri elekezi wa ujenzi huo, Mhandisi Andrian Eradius, alisema ujenzi huo unaendelea kwa maghorofa matatu yanayokadiriwa kuwa na uwezo wa kuhudumia familia 70 pamoja na sehemu za maduka kwa wananchi waliokuwa na miradi katika eneo hilo.

Mhandisi Adrian alisema ujenzi wa majengo hayo umefikia asilimia 98 na kazi inaendelea kwa sasa ni ya uwezekaji paa.

Aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada ilizochukua za kuwapa ushirikiano hasa katika changamoto iliyojitokeza na uhaba wa mchanga.

Alisema mradi huo ulipangwa kukabidhiwa serikalini mwezi huu, lakini kutokana na sababu za uwapo wa corona, mradi huo unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Balozi Seif alisema serikali imejizatiti kuimarisha makazi bora ya wananchi wake kwa ujenzi wa nyumba za kisasa ili kwenda sambamba na falsafa ya Chama cha Afro Shirazy Party (ASP) ya kuhakikisha ustawi wa jamii unaimarika katika kiwango cha kisasa.

Alisema fikra za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, katika kuona maendeleo ya makazi ya wananchi yanaimarika kwa kuzingatia mawazo ya Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume.

Alisema jitihada hizo za serikali zinaonyesha wazi kwamba maeneo yote ya Zanzibar mijini na vijijini kwa sasa yanakaribia kuwa na fursa na huduma zote muhimu.

Aliwahakikishia wananchi kwamba nyumba zinazojengwa zimelengwa kupewa wananchi waliovunjiwa nyumba zao katika maeneo hayo.

Waziri Balozi Ramia alisema wananchi wa Mtaa wa Kwahani ndio walengwa watakaofadikiwa na mradi huo.

Balozi Ramia alisema majengo hayo yatakapokamilika yatakuwa na uwezo wa kuhudumia familia 70, ingawa zilizopo kwenye kumbukumbu ni familia 40.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja cha Biashara kinauzwa Regent Estate Dsm mita za mraba 1300. Piga; 0693 689996, 0757 129546.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA CHETI



115892502

**Mwenye picha hapo juu, MASHAKA EMMANUEL MKAMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **Index No. S1803/0135/2017** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2017 kupitia LOWASA SEKONDARI. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye. Polisi taarifa: **ARU/ARU/RB/626803/2020.**

## JUDICIAL DECLARATION

**(Made Under Section 10 of Act No.59 of 1966 (R.E 2002)**

**I, JOHN HERMAN,** Adult, Christian and resident of Dar es Salaam, do hereby Make Oath and State as follows:-

1. That, I am the son of the late **AYUBU HERMAN** who died on 09/11/1998.
2. That, I am the Administrator of the estate of the late **AYUBU HERMAN** appointed on 23/12/2013 by Mwang'ombe Primary Court in Tanga region vide Probate Cause No. 68/2013.
3. That, I do recognize that during his life my late father own Land property Plot No.11 Block 64 B/B at Ngamiani in Tanga.
4. That, I am the custodian of various documents related to my late father's properties including Offer Letter document.
5. That, of recent I have realized that the said Offer Letter document as stated in Paragraph 4 above is lost or misplaced. Loss Report **DAR/KIJ/RB/55481/2020.**
6. That, in view of the above, I am in the process of looking to attain another or substituted Offer Letter document in respect of the said Landed property.

**WHEREFORE, I** make this declaration to be true to the best of my knowledge.

BEFORE ME:

NAME: DAUDI J. MALIMA

QUALIFICATION: ADVOCATE

115893302

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 102/2020**

**Ombi la NEEMA EZEKIEL MWAILUBI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu LYDIA EZEKIEL MWAMWENDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 24/8/2020.

115893402

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;263/2020**

**Ombi la REHEMA FESTO RUTASHOBYA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FESTO FEDNAND RUTASHOBYA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/09/2020.

Tarehe 8/9/2020

Sahihi ya Hakimu

215892902

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;265/2020**

**Ombi la JENITA NATHANI MWIFUNYI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JACOB LUPUMUKO MTWEVE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/09/2020.

Tarehe 8/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115893202

## KUPOTEA KWA CHETI



115893002

**TECLA STEPHEN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1049-0013** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. THOMAS AQUINAS** mwaka 2001. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAJ/RB/203/2020.**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 52/2020**

**MDAI NEEMA MGWILANGA**

**MDAIWA MEDADI NEBATI**

**Kwa MEDADI NEBATI**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba TALAKA**
Hivyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 21/09/2020 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 09/09/2020

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

115894002

## JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
09/09/2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **11-09-2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam** kuelekea **Tunduma** gari hilo lenye namba za usajili
**T 591 DQU / T 944 DPE**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 21 |
| **Upana** | - | mita | 3.4 |
| **Kimo** | - | mita | 5.4 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es salaam hadi Tunduma kupitia Vigwaza**

Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215893502

## JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
09/09/2020

**TANGAZO**

4. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **11-09-2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam kuelekea Tunduma** gari hilo lenye namba za usajili

**T 771 DMM / T 410 DDG**

5. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 21 |
| **Upana** | - | mita | 3.4 |
| **Kimo** | - | mita | 5.4 |

6. **Njia itakayotumika: Dar es salaam hadi Tunduma kupitia Vigwaza, Makambako**

Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215893502

## JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
09/09/2020

**TANGAZO**

7. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **11-09-2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Tunduma gari hilo lenye namba za usajili **T 863 DJT / T 825 BQF**
8. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 21 |
| **Upana** | - | mita | 3.4 |
| **Kimo** | - | mita | 5.4 |

9. Njia itakayotumika: Dar es salaam hadi Tunduma kupitia Vigwaza, Makambako

Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215893502

## KUPOTEA KWA CHETI



115893902

**EDITH RWIZA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0321-0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KINONDONI SEKONDARI** Novemba 1996. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/3905/07.**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA MOROGORO .**

**MAOMBI NA: 48 YA MWAKA 2020.**

**MLIGO KIRINGA KIMOTONGE...........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**HALIMA CHAMLULU**
**HUSSEIN SAID MOHAMED**
**MARIA PIUS NASSORO**
**FREDRICK MATEMBO**
**WILLFRED LUNDENGA**
**REHEMA JONAS.........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**HALIMA CHAMLULU**
**WILLFRED LUNDENGA**
**REHEMA JONAS**

Popote Mlipo unaarifiwa Mfike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 05/10/2020.Nyie wenyewe binafsi au mtume wawakilishi wenu bila kukosa ambapo MAOMBI yamepangwa kutajwa. Endapo hamtaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Majaribio ya chanjo corona yasitishwa

**LONDON, Uingereza**

MAJARIBIO ya mwisho ya kimatibabu kwa ajili ya chanjo ya virusi vya corona, yaliyotengenezwa na AstraZeneca pamoja na Chuo Kikuu cha Oxford yamesitishwa.

Usitishaji huo umetokana na mshiriki kuugua kutokana na athari za majaribio hayo.

AstraZeneca imeelezea kusitishwa kwa jaribio hilo, "kwa kawaida" pale inapotokea "kuugua kusiko eleweka".

Matokeo ya majaribio ya chanjo yanafuatiliwa kwa karibu kote duniani.

Chanjo ya AstraZeneca na Chuo Kikuu cha Oxford inaonekana kama yenye ushindani mkubwa wa makumi kadhaa ya chanjo zinazotengenezwa katika maeneo mengine ya duniani. Matumaini yalikuwa ya hali ya juu kwamba ingeweza kuwa moja ya chanjo za kwanza kuingia katika soko la chanjo, kutokana na mafanikio yake ya awali ya kipimo cha awamu ya kwanza na cha awamu ya pili.

Jaribio lake la kwenda awamu ya tatu katika wiki za hivi karibuni limewahusisha washiriki wapatao 30,000 nchini Marekani pamoja na Uingereza, Brazil na Afrika Kusini.

Majaribio ya awamu ya tatu ya chanjo kwa kawaida huwahusisha maelfu ya washiriki na yanaweza kudumu kwa miaka kadhaa.

Mhariri wa BBC wa masuala ya tiba, Fergus Walsh, aliripoti kuwa, vituo vyote vya majaribio ya kimataifa vimesimamishwa kwa muda, huku uchunguzi huru ukitathmini usalama wa takwimu kabla ya wadhibiti wa viwango vya chanjo kuamua kama jaribio hilo linaweza kuanza upya.

"Katika majaribio makubwa, ugonjwa unaweza kutokea kwa bahati lakini ni lazima utathminiwe na taasisi nyingine huru kuliangalia hili kwa uangalifu," Msemaji wa Chuo Kikuu cha Oxford alisema.

*BBC*




Maelfu ya waomba hifadhi katika kisiwa cha Lesbos cha nchini Ugiriki wamekimbia kunusuru maisha yao baada ya moto mkubwa kutokea kwenye kambi ya wahamiaji ya Moria. **PICHA: REUTERS**

# Mjadala mauzo dhahabu kuongezeka Uganda

**KAMPALA, Uganda**

KIWANGO cha mauzo ya nje ya dhahabu nchini Uganda kimeongezeka hadi kufikia mauzo ya thamani ya dola milioni 160 ndani ya mwezi Juni pekee, suala lililozusha mjadala.

Tayari zimeibuka tuhuma kuhusu vyanzo halisi vya dhahabu hiyo na kama ni halali au inatoka mataifa ya jirani na nchi hiyo.

Hata hivyo, mwandishi wa BBC, Isaac Mumena amenukuu takwimu za Benki Kuu ya Uganda, kwa mwezi wa Juni mwaka huu na kwamba taifa hilo lilisafirisha zaidi ya kilogramu 3,000 za dhahabu ikiwa ni mara mbili zaidi ya kiwango kilichosafirishwa mwezi uliopita.

Kuna mashaka huenda dhahabu hiyo inatokea nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) sehemu zilizokumbwa na vita na makundi ya waasi.

Mwezi uliopita Benki ya Dunia (WB) ilikadiria kiwango cha dhahabu haramu ya thamani ya dola milioni moja kilichosafirishwa kibiashara kupitia nchini Uganda.

Inadaiwa pia kuwa kutokana na janga la corona, wafanyabiashara wa magendo wanatumia ndege za kukodisha kusambaza vifaa vya huduma za afya kusafirisha dhahabu za magendo.

Serikali ya Uganda imekiri kuwa haiwezi kuzalisha kiasi kikubwa kama hicho, lakini kuwapo kwa mitambo ya kusafisha dhahabu kunasababisha kuwapo kwa kiwango cha juu, Kamishna wa Wizara ya Madini, Vincent Kedi ameeleza.

"Kiwango cha uzalishaji wa dhahabu nchini Uganda kimeongezeka ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita, pia tuna viwanda vitano vya kusafisha dhahabu na hivi vinasafisha dhahabu ya ndani na kutoka nje ya nchi hivyo usafirishaji wa dhahabu umeongezeka kutokana na hilo."

Kedi amekana kuwapo kwa dhahabu ya magendo kutoka mataifa jirani kama vile DRC ndiyo imesababisha kuongezeka kwa usafirishaji zaidi.

"Kwa sasa siwezi kusema ni kweli au ni uongo, ila ninachofahamu ni kwamba kiwanda cha kusafisha dhahabu kinasafisha dhahabu ya Uganda na ile inayotoka mataifa ya ukanda huu siyo DRC pekee ni pamoja na mataifa mengine kama Sudan na mataifa mbalimbali ya Afrika."

Naibu Mwenyekiti wa Kampuni ya AGR, Alphonse Katarebe, alisema tangu kuanzishwa kwa kampuni za kusafisha dhahabu nchini Uganda, kiwango cha uzalishaji kimepanda. Licha ya kuwa Uganda haina migodi mikubwa ya dhahabu, hivi karibuni madini yamekuja kuwa mojawapo ya bidhaa kwa masoko ya nje zinazoiletea fedha nyingi za kigeni hata kuliko zao la kahawa.

Hali hii imeleta ushindani mkali miongoni mwa wanaoshiriki biashara hiyo, huku wawekezaji kadhaa wakianzisha mitambo ya kusafisha dhahabu nchini ambako dhahabu huandaliwa kwa soko la kimataifa.

*BBC*

# Marekani kuondoa robo tatu ya jeshi Iran

**WASHINGTON, Marekani**

KAMANDA Mkuu wa Jeshi la Marekani, upande wa Mashariki ya Kati, Jenerali Kenneth McKenzie, ametangaza kuwa, nchi hiyo itaondoa zaidi ya robo tatu ya jeshi lake nchini Iraq ndani ya mwezi huu.

Jenerali McKenzie aliwaambia waandishi wa habari kuwa, jeshi litapunguzwa kutoka wanajeshi wapatao 5,200 mpaka 3,000 mwezi huu.

Hao watakaosalia wataendelea kuwashauri na kusaidia vikosi vya usalama vya Iraq kukabiliana na kundi la wapiganaji wa kiislamu la 'Islamic State (IS)'.

Mwezi uliopita, Rais Donald Trump alisema kuwa Marekani ina mpango wa kuondoa jeshi lake Iraq mapema iwezekanavyo.

Rais Trump anatarajiwa kuchukua hatua hiyo baada ya kutoa ahadi katika kampeni iliyopita kuwa anataka kuiondoa Marekani katika kile anachokieleza kuwa, vita isiyoisha.

Uwepo wa jeshi la Marekani limekuwa tatizo kubwa Iraq tangu nchi hiyo ilipohusika kumuua kiongozi wa ngazi ya juu nchini Iran, Qasem Soleimani, katika mapigano ya anga mjini Baghdad mwezi Januari.

Bunge la Iraq lilipitisha muswada wa kuondoa vikosi vya jeshi vya kigeni suala ambalo lilisababisha Rais Trump kutishia kufanya mashambulizi kadhaa dhidi ya Iraq.

"Tumewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika jeshi la anga huko. Kujenga msingi wake imetugharimu mabilioni ya dola. Hatutaondoka labda kama watatulipa gharama tuliyotumia," aliwaambia waandishi wa habari Januari 6, mwaka huu.

**BBC**

**Uwepo wa jeshi la Marekani limekuwa tatizo kubwa Iraq tangu nchi hiyo ilipohusika kumuua kiongozi wa ngazi ya juu nchini Iran, Qasem Soleimani, katika mapigano ya anga mjini Baghdad mwezi Januari.**

# GREENWOOD AOMBA RADHI ENGLAND




**LONDON, England**

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya England, Mason Greenwood amesema: "yeye mwenyewe ndiye wa kulaumiwa" baada ya kuondoshwa kikosini kwa kosa la kukiuka mwongozo wa karantini wa kujilinda na virusi vya corona akiwa nchini Iceland.

England ilicheza na Iceland Jumamosi na kuibuka na ushindi wa bao 1-0, ambao Greenwood alikuwa mmoja wa wachezaji aliyeichezea timu hiyo ya wakubwa kwa mara ya kwanza.

Mchezaji huyo wa Manchester United na kiungo wa kati wa Manchester City, Phil Foden, waliamriwa kuondoka kwenye kikosi hicho cha Kocha Gareth Southgate siku ya Jumatatu wakati wakijiandaa na mchezo wa Jumanne.

Greenwood alisema: "Ninaweza tu kuomba msamaha kwa aibu niliyoisababisha."

Aliongeza: "Hususani, ninataka kumwomba radhi Gareth Southgate, kwa kumwangusha, wakati alionyesha kuniamini kwa kiasi kikubwa.


"Kuichezea England ilikuwa moja kati ya nyakati za kujivunia sana katika maisha yangu na ni mimi pekee ninayepaswa kulaumiwa kwa kosa hili kubwa.

"Ninaiahidi familia yangu, mashabiki, Manchester United na England kuwa hili ni somo nitajifunza."

Kwa mujibu wa ripoti za Iceland na vyombo vingine, Foden na Greenwood walidaiwa kukutana na wanawake wawili katika sehemu tofauti za hoteli mbali na mahali kikosi cha England kilipokuwa kinakaa.

Southgate amewaelezea wachezaji hao kuwa 'wajinga' akiongeza kuwa: "Ni suala kubwa sana na tumelishughulikia namna hiyo na tumechukua hatua haraka sana kadiri tulivyoweza."

## Lacazette: Sifikirii kuondoka Arsenal




**LONDON, England**

ALEXANDERE Lacazette amewaambia mashabiki wa Arsenal kwamba hafikirii kabisa kuachana na timu hiyo na bado ataendelea kuwa hapo kwenye dimba la Emirates.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa, alidhaniwa atakuwa mmoja wa wachezaji wa Arsenal ambao kocha Mikel Arteta atawapiga bei, ili kupata fedha za kusajili wachezaji wapya.

Juventus walitajwa kufukuzia huduma ya mshambuliaji huyo baada ya Gonzalo Higuain kufunguliwa mlango wa kutokea.

Lacazette pia alidaiwa kupelekwa kama ofa huko Atletico Madrid ili kuwalainisha wamwachie kiungo mkabaji, Thomas Partey, anayetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 44.

Shabiki mmoja alitumia ukurasa wake wa Instagram kumwomba mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon abaki Arsenal, wakati alipoandika: "Neno moja. BAKI."

Lacazette alijibu ujumbe huo wa shabiki kwa kuweka 'emoji' ya kukonyeza. Kwenye kikosi cha Arsenal, fowadi huyo alifunga mabao 10 katika mechi 30 kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita.

## Barca yafunguka kuhusu Umtiti

**BARCELONA, Hispania**

KLABU za Manchester United na Arsenal zimeambiwa kwamba, Samuel Umtiti atapatikana bure tu baada ya Barcelona kujiandaa kufungua milango ya kuachana naye.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, mlinzi huyo raia wa Ufaransa, mkataba wake pale Nou Camp utafika tamati mwaka 2023, lakini mabosi wa timu hiyo wanataka kuachana naye bila ya kupata chochote.

Umtiti hana nafasi kwenye kikosi cha Barcelona baada ya namba kuchukuliwa na Mfaransa mwenzake, Clement Lenglet, huku majeraha ya mara kwa mara yakimtibulia mambo yake.

Beki huyo wa kati alicheza mechi 13 tu za La Liga msimu uliopita wakati Barcelona ilipotema ubingwa huo kwa mahasimu wao Real Madrid. Kikosi hicho kwa sasa kipo chini ya kocha mpya, Ronald Koeman.

Kocha huyo Mdachi, tayari ameshamwondoa Ivan Rakitic na amemwambia straika Luis Suarez na kiungo Arturo Vidal kwamba hawapo kwenye mipango yake ya baadaye.

Rakitic alikubali kukatwa mshahara wake ili kurudi kujiunga na Sevilla, wakati Juventus inaripotiwa kuwa kwenye milango ya kumchukua Suarez kama atafuzu mambo mengi ikiwamo lugha ya Kitaliano.

Na Umtiti anaweza kufunguliwa mlango wa kutokea huku klabu kibao za Ligi Kuu England ikiwamo United na Arsenal zinahitaji saini yake.



HABARI MICHEZO



# GIROUD
## AKARIBIA REKODI YA HENRY

**PARIS, Ufaransa**

OLIVIER Giroud alifunga bao lake la 40 la kimataifa wakati Ufaransa ikiifunga Croatia magoli 4-2 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA, katika mchezo ambao ulikuwa ni kama marudiano ya fainali ya Kombe la Dunia la mwaka 2018, uliopigwa Jumanne usiku.

Straika huyo wa Chelsea, Giroud mwenye umri wa miaka 33, alifikisha mechi yake ya 99 na akafunga kwa penalti wakati akitokea benchi na kubakiza goli moja tu kumfikia gwiji wa Ufaransa, Michel Platini.

Gwiji wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwa timu hiyo ya Ufaransa akiwa na mabao 51.

Mlinzi wa zamani wa Liverpool, Dejan Lovren alianza kuwaweka mbele Croatia, lakini mabingwa hao wa dunia haraka wakarudi kwa kasi mchezoni.

Fowadi wa Barcelona, Antoine Griezmann alisawazisha na straika wa Manchester United, Anthony Martial akafunga la pili kwa shuti lililomshinda golikipa, Dominik Livakovic.

Josip Brekalo akasawazisha, lakini mabao kutoka kwa Dayot Upamecano na Giroud yakaipa ushindi huo Ufaransa ambao sasa wanapointi sawa na Ureno kileleni mwa kundi la 3.

Eduardo Camavinga ambaye aliingia dakika ya 63 aliweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea Ufaransa, akiwa na umri wa miaka 17 na siku 303, tangu Maurice Gastiger aliyeiweka Februari mwaka 1914.



## JUVENTUS YAJITOSA KUMSAJILI TRAORE

**LONDON, England**

JUVENTUS imetoa ofa ya kutaka kumsajili nyota wa Wolves, Adama Traore kwa wakala wake, Jorge Mendes, kwa mujibu wa Calciomercato.

Winga huyo wa Wolves amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa kubwa Ulaya, lakini Juventus ndio wanaonekana wanaweza kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania.

Juve, Liverpool, Manchester City, Real Madrid na Barcelona zimekuwa zikimwania kumsajili Traore katika siku za hivi karibuni.

Traore amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi katika misimu miwili iliyopita akicheza pale Wolves kwenye Ligi Kuu England na kuifikisha michuano ya Ligi ya Europa.

Zao hilo la Barcelona, alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake hiyo ya utotoni, lakini sasa Juventus inaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumtwaa.

Traore anaweza kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 70 pamoja na kumtoa Douglas Costa na Federico Bernardeschi.

# De Bruyne mwanasoka bora wa mwaka EPL

**LONDON, England**

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne ameshinda tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa Ligi Kuu England msimu wa 2019-20.

City iliachia taji lake la Ligi Kuu kwa Liverpool wakati walipomaliza msimu wakiwa nyuma ya pointi 18 dhidi ya kikosi cha Jurgen Klopp, lakini De Bruyne alifurahia mafanikio makubwa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho 23 katika mashindano yote, akiifikia rekodi ya Thierry Henry ya asisti 20 kwa msimu mmoja wa Ligi Kuu England.

De Bruyne aliwapita mchezaji mwenzake, Raheem Sterling, pamoja na nyota wawili wa Liverpool, Jordan Henderson, Virgil van Dijk, Sadio Mane na Trent Alexander-Arnold.

Mlinzi wa kulia wa England, Alexander-Arnold alipata tuzo ya mchezaji bora kijana wa mwaka.

De Bruyne, ambaye ni mchezaji wa kwanza wa City kushinda tuzo hiyo, alisema: "Ni heshima kubwa kwangu. Kuchaguliwa na wenzangu kutoka kwa washindani wetu na kuwa mchezaji bora wa mwaka.


"Ni jambo zuri zaidi kwamba mimi ndio mchezaji wa kwanza wa City kupata tuzo hii, kwa hakika ni heshima kubwa kwangu na kwa klabu."

Pia katika tuzo hiyo, kilitajwa kikosi bora cha mwaka ambacho: Nick Pope (Burnley); Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Caglar Soyuncu (Leicester City), Virgil van Dijk (Liverpool), Andy Robertson Liverpool); Kevin De Bruyne (Manchester City), Jordan Henderson (Liverpool), David Silva (Manchester City, now at Real Sociedad); Sadio Mane (Liverpool), Jamie Vardy (Leicester City) na Pierre-Emerick Aubameyang (Arsenal).



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AZIDI KUNG'ARA ULAYA

**Ni baada ya nahodha na mshambuliaji huyo wa Ureno kuweka rekodi ya kufunga mabao 100 kwa nchi yake...**

**LISBON, Ureno**

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza wa Ulaya kufungia nchini yake ya Ureno mabao 100 ya kimataifa kwenye mechi za soka za wanaume, wakati akifunga mabao mawili katika mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Sweden, Jumanne usiku.

Ronaldo sasa amefikisha mabao 101 aliyofunga katika mashindano ya kimataifa akiwa na kikosi cha Ureno.

Nahodha huyo wa Ureno alifunga bao la kwanza katika dakika ya 57 kwa shuti la adhabu ndogo na kufikisha idadi hiyo ya mabao 100.

Halafu fowadi huyo wa Juventus mwenye umri wa miaka 35, akafunga la pili nje ya 18 na kufikisha mabao 101.

Ronaldo, ambaye alicheza kwa dakika 81, amebakiza mabao nane kuifikisha rekodi ya ufungaji bora ya dunia.

Mchezaji wa zamani wa Iran, Ali Daei ndiye mchezaji pekee duniani aliyefunga mabao mengi zaidi ya kimataifa kuliko Ronaldo - akiwa na mabao 109 aliyoifungia nchini yake kati ya mwaka 1993 na 2006.

Mchezaji anayefuata kwa sasa ni Sunil Chhetri wa India mwenye mabao 72 na Lionel Messi wa Argentina mwenye mabao 70.

Matokeo hayo yana maana kwamba bingwa huyo mtetezi wa Kombe la Ligi ya Mataifa ya UEFA, Ureno, imeshinda mechi zake zote mbili za ufunguzi mwaka huu katika mashindano hayo.

Ushindi huo kwao ulionekana kuwa rahisi baada ya Gustav Svensson wa Sweden kutolewa nje kwa kadi nyekundu, lakini wao Ureno walimpoteza nyota wa Manchester City, Bernardo Silva aliyeumia.

Ureno wangeweza kupata mabao mengi zaidi kama shuti la Bruno Fernandes lisingegonga mwamba na Ronaldo ambaye hiyo ilikuwa mechi yake ya 165, shuti lake liliokolewa na golikipa, Robin Olsen.

Karibia nusu ya mabao ya Ronaldo ya kimataifa yamekuja baada ya kutimiza umri wake wa miaka 30 ambapo amefunga jumla ya mabao 49 kati ya 47.

## KWA UFUPI

### DRAXLER ATAKIWA LEEDS

LEEDS United inajaribu kupambana kunasa saini ya winga wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Julian Draxler (26), ili kujiunga na klabu yao. ***(RMC Sport - in French)***

### STONES KUBAKIA CITY

BEKI wa kati wa Timu ya Taifa ya England, John Stones (26), anajiandaa kubakia kwenye klabu ya Manchester City na anatarajia kupambana kusaka namba kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Pep Guardiola. ***(Telegraph)***

### TOMORI ANUKIA EVERTON

BEKI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Fikayo Tomori, ambaye ana umri wa miaka 22, anakaribia kukamilisha mchakato wa kujiunga kwa mkataba wa muda mrefu wa mkopo na Everton. ***(ESPN)***

### BARCA YAMTAKA GARCIA

BARCELONA iko tayari kuwania saini ya beki wa Manchester City Mhispania, Eric Garcia, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### BROOKS AKARIBIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inatajwa kuwa kwenye nafasi nzuri ya kunasa saini ya winga wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Wales, David Brooks (23) ukilinganisha na wapinzani wao kwenye mchakato huo, Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### ROMERO AWEKWA SOKONI

MANCHESTER United iko tayari kupokea ofa ya kumuuza golikipa wa timu ya Taifa ya Argentina, Sergio Romero, ambaye ana umri wa miaka 33, na tayari Aston Villa na Chelsea zimeonyesha nia ya kumhitaji. ***(Express)***

### WOLVES KUMBANA SANTO

MABOSI wa Wolves wanajipanga kuanza mazungumzo na kocha wake Mreno, Nuno Espirito Santo kuhusiana na kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu. ***(Sun)***

### BREWSTER NJIA NYEUPE

LIVERPOOL imeridhia kumuuza straika wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ya England, Rhian Brewster (20), katika majira ya joto lakini ikiweka kipengele cha kumnunua tena. ***(Sky Sports)***

### ROSE KUONDOKA SPURS

BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Dany Rose (30), anajiandaa kuondoka Tottenham lakini ameweka wazi atapenda kujiunga na klabu ya nje ya nchi hiyo. ***(Sun)***

### ARSENAL YAMFUATA AREOLA

ARSENAL imewasilisha ofa ya kumsajili kwa mkopo wa muda mrefu, golikipa wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alphonse Areola (27), ambaye sasa yuko kwenye kikosi cha Paris St-Germain. ***(Mirror)***

### MARTINEZ KUTUA VILLA

ASTON Villa inataka kukamilisha haraka mchakato wa kumsajili golikipa wa Arsenal na Argentina, Emiliano Martinez (28), ili aweze kuwahi mechi ya kwanza ya msimu huu itakayochezwa Jumapili. ***(Mail)***

### BOURNEMOUTH YAJIPANGA

MABOSI wa Bournemouth wamewasilisha ofa ya kumsajili beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Marekani, Cameron Carter-Vickers (22), kwa mkopo pamoja na mshambuliaji wa Stoke City, Tyrese Campbell, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# MTIBWA SUGAR YAJIPANGA KUIBANIA SIMBA JAMHURI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema atahakikisha kikosi chake kinafanya vizuri katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya Simba itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

Katwila aliliambia gazeti hili, wamejipanga kutoruhusu kufungwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, ili kujiweka kwenye mazingira salama katika msimu huu ambao umeanza wiki iliyopita.

Kocha huyo alisema tayari ameshaanza kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo wao wa ufunguzi dhidi ya Ruvu Shooting, na kila mchezaji amejiandaa kutorudia makosa pale watakapowakaribisha mabingwa watetezi, Simba.

Alisema msimu uliopita amekuwa na historia ya kupoteza pointi mbele ya Simba, hivyo hataki kuona hali hiyo inajirudia tena.

"Maandalizi yetu yapo vizuri, sio kwa ajili ya mchezo dhidi ya Simba, tumejipanga kutafuta alama muhimu katika kila mechi, tumepata pointi moja na Ruvu, sasa akili na nguvu zetu ni kuhakikisha tunapata alama zote kwa mpinzani wetu anayefuata," alisema Katwila.


Alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani, na wanaiheshimu Simba ambayo haijafanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake kilichoshiriki msimu uliopita.

"Malengo yetu ni kuhakikisha msimu huu tunatumia vema uwanja wa nyumbani, tutakuwa tunashuka uwanjani kupambana, ili kuondoka na ushindi tu, unapochukua alama au ushindi kwenye michezo ya nyumbani, hujiweka kwenye mahali salama mapema," Katwila alisema.

Alieleza kila mchezo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ni muhimu, hivyo amewaandaa wachezaji wake kuongeza umakini.

"Kila mechi kwetu ni muhimu, unaweza kusema ni fainali, tunataka kuwa kwenye mbio za ubingwa, hivyo tunahitaji kupata matokeo mazuri kila tunapocheza, naamini hilo linawezekana," aliongeza kocha huyo.

Kikosi cha Simba kiliingia kambini jana na kinatarajia kwenda Morogoro mapema, ili kuwavaa wenyeji wao Mtibwa Sugar.




Meneja Uhusiano wa SportPesa Tanzania, Sabrina Msuya (kushoto), akimkabidhi hundi ya Sh. milioni 20.1, mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Abdulsalaam Juma, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya mechi za mpira wa miguu wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamisaa wanawake kunolewa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KUELEKEA msimu mpya wa 2020/21, Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), linatarajia kuendesha mafunzo kwa makamisaa wanawake itakayofanyika leo kwenye ukumbi wa Mau Ze Dong, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya ZFF, ambaye kamisaa wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Muhsini Ali Kamara, alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuwatayarisha, ili wasimamie mechi za Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu. Kamara alisema mafunzo hayo yatashirikisha wachezaji wa soka waliostaafu, pamoja na waandishi wawili wa habari za michezo wa visiwani hapa.

Alisema katika mafunzo hayo watatoa darasa kuhusiana na sheria 17 za mpira wa miguu na kanuni na majukumu anayotakiwa kufanya kamisaa, anaposimamia mchezo husika.

"Mafunzo haya yanafanywa katika muda muafaka kwa sababu ZFF imedhamiria kuwapo kwa ligi endelevu ya wanawake na tumejipanga zaidi kuwaendeleza wanawake ili wafikie malengo," alisema Kamara.

Aliongeza, anaamini baada ya mafunzo hayo, idadi ya makamisaa wanawake itaongezeka na kutaja kwa sasa Zanzibar ina makamisaa wa jinsia hiyo wawili tu.

Aliwataka pia wanawake kujitokeza kwa wingi katika mafunzo na semina mbalimbali ikiwamo ya makocha, waamuzi na ya madaktari wa michezo ili kwenda sambamba na soka la sasa la dunia.

## Mashabiki Mbeya City FC watulizwa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City imewataka mashabiki wake kutulia na kueleza upungufu uliyojitokeza katika mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya KMC FC yatarekebishwa na timu yao itarejea kwenye ushindani.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Emmanuel Kimbe alisema hayo kufuatia matokeo ya kubugizwa mabao 4-0 dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, na kuzua maswali mengi kwa mashabiki wa Mbeya City.

Kimbe alisema, kucheza ligi ndefu na kuwa na muda mfupi wa usajili na maandalizi ndiyo sababu kubwa iliyofanya timu hiyo kutofanya vema katika mechi yake ya kwanza, lakini hayo yote yanafanyiwa kazi na wataingia uwanjani tofauti kwenye mchezo wa raundi ya pili.

"Sisi tulicheza ligi ndefu kuliko timu nyingine yoyote kwa sababu tulifika hadi kwenye mechi za mchujo wakati wenzetu wakiwa wameshamaliza ligi, hivyo tukawa na muda mfupi kwenye usajili na maandalizi pia japo tuna wachezaji wazuri," alisema Kimbe.

Aliongeza anaamini timu yao itakaa vizuri baada ya muda si mrefu na anawataka mashabiki wa Mbeya City ambao wameonekana kushtushwa na kipigo hicho kujiandaa kupokea matokeo chanya.

Mbeya City ambayo kwa sasa inakamata mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu bado iko jijini Dar es Salaam, ikijiandaa na mchezo wa raundi ya pili dhidi ya Yanga utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa.

## Cheka atamba kumchapa Mmalawi

**Na Adam Nyangasa, TUDARCO**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Cosmas Cheka, amesema yupo 'fiti' kuelekea pambano lake dhidi ya mpinzani wake kutoka Malawi, Phiri Hannoch litakalofanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

Pambano hilo litakuwa la raundi 12 na ni la kuwania ubingwa wa UBO la uzito wa Welter.

Akizungumza na gazeti hili jana, Cosmas alisema amefanya mazoezi katika kiwango cha juu, ili kuhakikisha anafanya vizuri na vile vile anatoa burudani kwa Watanzania watakaofika kuhudhuria pambano hilo.

Cosmas alisema lengo la kusaka ushindi katika pambano hilo, ni kuipa heshima nchi na kupeperusha vema bendera ya taifa katika mchezo wa ngumi.

"Nawashukuru makocha wangu wote wanaondelea kuniandaa vizuri na kikubwa ninamwomba Mungu aniwezeshe, ili kufanikisha malengo yangu, nimejipanga kuondoka na ushindi," alisema Cosmas.

Bondia huyo ambaye ni mdogo wake bondia maarufu, Francis Cheka, alisema anataka kuendeleza rekodi nzuri, hivyo alianza mapema maandalizi ya pambano hilo la kimataifa.

Hata hivyo alikataa kueleza atamaliza pambano hilo katika raundi ya ngapi, kwa sababu anaamini mpinzani wake pia amefanya maandalizi ya kuwania ubingwa wa mkanda huo.

Michezo
Alhamisi Septemba 10, 2020
Nipashe



RONALDO AZIDI KUNG'ARA ULAYA HABARI UK 22

## YANGA YAANDAA 'DOZI' MAALUMU

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema wameandaa programu maalumu kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi zao zinazofuata ikiwamo dhidi ya Mbeya City itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Zlatko alisema kwa sasa anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyaona katika mechi ya kwanza kwa lengo la kuhakikisha wanaibuka na ushindi Jumapili.

Kocha huyo alisema timu yake bado ni mpya na anahitaji muda mfupi wa kutengeneza muunganiko mzuri ambao utamsaidia kufanikisha ushindi na anaamini mechi inayofuata wataingia wakiwa imara zaidi.

**"Timu haikuwa na muda mrefu wa maandalizi, tunatumia muda huu uliopo kujiandaa na kujenga kikosi imara, pia kujenga muunganiko wa wachezaji, tutakuja kufanya vizuri mbele katika mechi zetu zijazo," alisema Zlatko.**

Alieleza timu yake haikuwa na katika kiwango bora katika kipindi cha kwanza kwenye mchezo wao dhidi ya Tanzania Prisons, lakini walishindwa kutumia vema nafasi zote walizopata.

"Baada ya kuona wachezaji hawako 'fiti' na tatizo la pumzi ambalo linawafanya wanashindwa kumudu kucheza dakika 90, nimeshaanza kutatua tatizo hili, pia wanatakiwa kuongeza utulivu na umakini," Zlatko alisema.

Alisema wana nafasi ya kufanya vizuri katika mechi zinazofuata kutokana na kupata muda zaidi wa kuwanoa tofauti na alivyoikuta timu, siku chache kabla ya msimu mpya haujaanza.

Mechi ya kwanza ya mashindano ya kocha huyo aliyepokea mikoba ya Luc Eymael ilikuwa ni Septemba 6, mwaka huu, ambapo ilikuwa dhidi ya Tanzania Prisons ya Mbeya ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.

# MO DEWJI: SIONDOKI SIMBA SC

## •••Mwekezaji huyo atangaza kubakia klabuni hapo, labda wanachama wafanye uamuzi mwingine wa...



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam, Mohammed Dewji 'Mo'. **PICHA: MAKTABA**

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Simba ikitarajia kuiwakilisha tena Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo', amesema hataacha kuwekeza ndani ya timu hiyo licha ya kukutana na changamoto mbalimbali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mo, alisema kuwa hafikirii kuondoka katika klabu hiyo na ataendelea kuhakikisha inapata mafanikio, huku mabadiliko ya mfumo wa uendeshwaji yakiendelea kufanyiwa kazi.

Mo alisema Simba ni timu anayoipenda kwa dhati na ataendelea kuweka fedha zake kwa sababu ya kusaka mafanikio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Alisema kwa sasa bajeti ya Simba kwa mwaka ni Sh. bilioni saba na mwaka huu alitumia kiasi cha bilioni 1.9 kwa ajili ya kusajili wachezaji wa timu hiyo.

Alieleza kuwa hafikirii kuondoka katika klabu hiyo ya Wekundu wa Msimbazi labda pale wanachama wa klabu hiyo watakapohitaji afanye uamuzi huo.

"Ninapenda kusema kuwa wazi mimi siondoki Simba, labda wenye Simba yao watake," Mo alisema hayo kwa kifupi.

Mfanyabiashara huyo alisema awali kabla ya kurejea Simba, bajeti yake ilikuwa ni Sh. milioni 600, lakini kwa sasa bajeti hiyo imefikia Sh. bilioni saba anazilipa yeye kutoka katika kampuni zake mbalimbali.

"Bajeti ya Simba imepanda karibu mara 10, mambo yanakwenda sawa sawa, tumesajili wachezaji wa kiwango cha juu, tumeshaanza kufika walipo T.P Mazembe na tutaelekea walipo Al Ahly ambao wanasajili mchezaji hadi kwa bilioni moja," Mo aliongeza.

Aliwataka mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi na wadau wengine wa mpira wa miguu kuendeleza mshikamano kwa sababu Simba itakapofanya vizuri, itazibeba klabu nyingine katika kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa Tanzania kutoa zaidi ya timu moja.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa klabu hiyo iliwahi kupita kwenye wakati mgumu kwa kukosa fedha za kujiendesha, hali ambayo sasa imemalizika.

Manara alisema kwa sasa Simba inaendeshwa kisasa na imekuwa mfano wa kuigwa kwa klabu mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania.

Aliongeza kikosi cha timu hiyo kitaondoka jijini leo na kuelekea Morogoro kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walianza msimu mpya ugenini Mbeya kwa kuwakabili Ihefu FC na baada ya mechi ya keshokutwa itarejea jijini kuwakaribisha Biashara United ya Musoma ifikapo Septemba 20, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >